# Mashekhe Uamsho walivyotua Z'bar usiku

**Na Waandishi Wetu**

FURAHA imetawala kwa familia za viongozi wa Jumuiya ya Uamsho na Mihadhara ya Kiislamu Zanzibar walioachiwa huru baada ya kukaa rumande kwa muda wa miaka saba bila ya kuhukumiwa wakikabiliwa na tuhuma za ugaidi.

Viongozi hao walifika katika familia zao juzi majira ya saa tatu usiku bila ya familia zao kuwa na taarifa kuwa jamaa zao wameshaachiwa huru.

Mahakama Kuu imewaachia huru viongozi hao 36 baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini kuwasilisha hati ya kuonyesha hana nia ya kuendelea na shauri hilo.

Kesi hiyo ilikuwa ikisikilizwa mbele ya Jaji Mustaph Ismail na washtakiwa walikuwa wakitetewa na jopo la mawakili akiwamo Juma Nassoro.

Wakili Nassoro aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa alipata taarifa ya kuachiwa kwao na wakaamua kwenda gerezani walikopata taarifa hiyo na walipokwenda mahakamani, walikuta hati iliyotoka kwa DPP.

"Kweli wameachiwa, wengine wamesharudi Zanzibar, tulikuwa hatuna taarifa, tuliposikia tulifuatilia na kupata taarifa kwamba waliachiwa," alidai.

Washtakiwa hao walikuwa wanakabiliwa na mashtaka 11 baada ya mengine kufutwa, wakidaiwa kutenda makosa ya ugaidi kati ya Machi na Juni, 2014 Tanzania Bara.

Pia wanadaiwa kula njama, kufanya mikutano ya ugaidi, kutaka kumuua Shekhe Kassim Mafuta na kufanya mikutano ya ugaidi Kibiti.

Viongozi hao ni Sheikh Farid Hadi Ahmed, Mselem Ali Mselem na wenzao 34 ambao mashtaka yaliondolewa kwa sababu DPP ameona ushahidi uliobaki baada ya mashtaka mengine kufutwa ni uhalifu ambao hauwezi kuwatia hatiani.

Ushahidi wa mashtaka uliyobaki ulikuwa unaungana na mashtaka yaliyofanyika Zanzibar ambayo yamefutwa.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, viongozi hao wameachiwa kwa kuwa ameona hawezi kuendelea na mashtaka yaliyobaki dhidi yao.

Mbali na Sheik Farid na Mselem, viongozi wengine ni Kassim Salum Nassoro, Abdallah Said Ali maarufu Madawa, Nassoro Hamad Abdallah, Hassan Bakari Suleiman, Antar Hamoud Ahmed na Mohamed Ishaka Yussuf.

Wengine ni Rashid Ali Nyange maarufu Mapara, Salum Amour Salum, Suleiman Othman Maulid, Kassim Mkadamu Khamis, Salum Ali Salum, Haroub Rashid Ally, Abdallah Omary Mzee, Hassan Hamis Hamiss maarufu Mbera na Mgeni Alli Omary maarufu Master Mgeni.

Pia wamo Kachelo Koplo mstaafu wa Jeshi la Polisi, Hamis Mohamed maarufu Al Qaeda au Hamisi wa Uzi, Tesha Rwiza maarufu kama Murshid au Abuu Katada, Twaha Said Katundu maarufu Dk. Gwalubu au Adam Twalibu na Ally Khamis Ally.

Washtakiwa wengine ni Sharif Suleiman Sharif maarufu kama Shehe Sharif, Jamal Nurdin Swaleh, Abdallah Hassan Hassan maarufu kama Jibaba, Hussein Mohamed Ali, Juma Sadala Juma, Said Kassim Ali, Khamis Amour Salum na Said Amour Salum.

Wengine ni Abubakar Ibrahim Mngodo, Salum Ali Salum maarufu Al Qaeda, Alawi Othman Abeid, Amir Khamis Juma, Said Shehe Sharrif, Ally Mwinchande Said na Mohamed Miraj Ibrahim.

Mashekhe walioachiwa juzi wakiwamo Shekhe Farid Hadil Ahmed na Mselem Ali ambao serikali iliwasafirishwa kutoka Dar es Salaam hadi visiwani Zanzibar kwa familia zao.

**GEREZANI HADI ZANZIBAR**

Akizungumza na waandishi wa habari visiwani Zanzibar jana, mdogo wa Shekhe Farid, Awadhi Hadi Ahmed, alisema kwa muda wote kaka yao akiwa gerezani, waliishi katika maisha ya unyonge na huzuni.

Alisema kuwa wamefarajika kuona kaka yao ametoka gerezani na kujumuika nao pamoja, jambo ambalo hawakulitarajia.

"Jana (juzi) usiku ghafla tunasikia mlango unagongwa, tulipofungua tunamwona kaka yetu Shekhe Faridi," alisema akiwa nyumbani kwao eneo la Betras mjini Unguja.

Mtoto wa Shekhe Farid, Muaadh Farid Hadi (21), alibainisha kuwa wakati baba yake anawekwa mahabusu gerezani, alikuwa na umri mdogo na hakujua kilichokuwa kinaendelea na amefurahi kuonana na baba yake.

"Ninafuraha sana leo hii kuonana na baba yangu ambapo leo (juzi) ni siku yangu ya kuzaliwa, ninatimiza miaka 21, hivyo nina furaha nyingi sana," alisema.

**ALIYEACHIWA ALONGA**

Shekhe Mselem Ali ambaye ni miongoni mwa mashekhe walioachiwa huru juzi, alisema waliondoka gerezani majira ya saa moja usiku na kupelekwa uwanja wa ndege kwa ajili ya safari ya kurudi Zanzibar.

Alieleza kuwa ndege waliotumia haikuwa na watu wengi na walipofika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, walishukia eneo la wasafiri maalum (VIP).

"Baada ya kufika kiwanja cha ndege Zanzibar, kila mmoja, mimi na Shekhe Farid tuliingizwa kila mmoja na gari yake, mimi niliulizwa Mselem tukupeleke kwa mke wako mkubwa au mdogo mimi nikawaambia wanipeleke nyumbani kwetu kwa mama yangu mzazi maana hatujaonana," alisema Shekhe Mselem.

Aliwapongeza viongozi wa nchi, akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Mwinyi kwa busara na hekima zao na hatimaye kuachiwa huru. Aliwataka wananchi watulie na furaha yao itoshe kuwa wapo huru na kuendelea kuhubiri amani ya nchi.

Alisema serikali itakapowaruhusu kufanya mikusanyiko, watakutana na wananchi lakini wasiporuhusiwa hawatafanya na wataheshimu uamuzi wa serikali. Aliwataka wananchi kuendelea kuwaombea dua viongozi wa nchi kwa sababu wanapita katika wakati mzito na wanahitaji busara, uadilifu na hekima."Mungu awabariki sana viongozi wetu wa nchi akiwamo Mama Samia na Rais Dk. Mwinyi kwa busara zao na tulipokua gerezani kipindi hiki cha uongozi wa Mama Samia tulikuwa tukitembelewa na viongozi mbalimbali ambapo huko nyuma haikuwahi kutokea," alisema.

Shekhe Farid alisema kuachiwa kwao kunatokana na busara na hekima za Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi na Rais wa Tanzania, Samia.

Alisema viongozi hao wa nchi ni imara na watiifu, hivyo aliwaomba wananchi kuwaombea dua kuendelea kuiongoza nchi kwa amani na utulivu. Hata hivyo, aliwaomba viongozi hao kuendelea kutumia busara zao kwa kuwaokoa watu wengine ambao wamewekwa gerezani kwa muda mrefu bila ya kesi zao kusikilizwa na kutolewa hukumu.

"Pale gerezani kuna watuhumiwa wapatao 220 ambao kesi zao hazijasikilizwa na sheria hazijafuatwa

"Mfano yupo mzee wa miaka 96 yupo pale anatuhumiwa kwa kesi ya ugaidi, tunaiomba serikali itumie busara ipitie kesi zao," alisema.

Alisema kuna haja serikali kutumia busara kwa kuwa wamepoteza mali zao nyingi wakati walipokuwa gerezani.

■**Imeandikwa na Kulwa Mzee (DAR) na Rahma Suleiman (ZANZIBAR)**

# Seth wa IPTL aachiwa huru

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imemwachia huru Mkurugenzi wa Kampuni ya Kufua Umeme (IPTL), Herbinder Seth, kwa masharti ya kutotenda makosa tena na atakuwa chini ya uangalizi wa mwaka mmoja baada ya kukiri makosa yake na kukubali kulipa Sh. bilioni 26.9.

Seth alitoka eneo la mahakama huku akiwa amezingilwa na ndugu na jamaa waliofika mahakamani hapo akiwamo ndugu yake waliofanana hali iliyowachanganya waandishi wa habari na wananchi wengine kubaini yeye ni yupi kati yao.

Seth alitokea mlango wa nyuma ya mahakama na gari lililombeba lilikuwa limeegeshwa maeneo ya mlango.

Hukumu ya mahakama ilitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, baada ya mshtakiwa huyo kufikia makubaliano na DPP ya kukiri makosa yake na kukubali kulipa fidia.

Alisomewa shtaka jipya la kujipatia Dola za Marekani 22,198,544.60 na fedha taslimu Sh. 309,461,300,158.27 kwa njia ya udanganyifu.

Baada ya kukiri kosa hilo mahakama ilimtia hatiani na kutoa nafasi kwa upande wa Jamhuri na utetezi kumzungumzia mshtakiwa kabla ya mahakama kutoa adhabu.

Wakili wa Serikali Mkuu, Martenus Marando, alidai mahakamani hapo kuwa hakuna kumbukumbu kwamba mshtakiwa ana makosa mengine aliyowahi kufanya.

"Tunaomba mshtakiwa alipe fedha alizokubali katika mkataba Sh. 26,946,487,420.80 ndani ya miezi 12 ambapo kati ya hizo jana Juni 16, alifanikiwa kulipa fidia ya Sh. milioni 200," alidai na kuomba apewe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Wakili wa mshtakiwa, Melchizedek Lutema aliomba mteja wake apewe adhabu ndogo, ni mkosaji wa mara ya kwanza, ana matatizo ya afya na amekaa rumande kwa miaka minne.

Akitoa adhabu, Hakimu Shaidi alisema amezingatia hoja za pande zote mbili, mshtakiwa ni mkosaji wa mara ya kwanza na amekaa rumande muda mwingi wa kutosha, ameona na kujifunza mengi.

Alisema mshtakiwa alikubali kwa hiari kuingia makubaliano ya kumaliza kesi kwa njia ya muafaka ambayo haiumizi upande wowote.

"Kwa kuzingatia hayo mahakama inakuachia huru kwa masharti ya kutotenda kosa la jinai tena na utakuwa chini ya uangalizi mwaka mmoja," alisema Hakimu Shaidi.

Alisema mahakama ilitoa uamuzi huo ili kumpa nafasi mshtakiwa ya kutimiza makubaliano waliyofikia.

Pia Hakimu Shaidi, alisema hati za kusafiria za mshtakiwa zishughulikiwe kiutawala na endapo utatokea ugumu upande wa utetezi wawasilishe maombi mahakamani.

Kabla ya hukumu, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alisoma mkataba waliokubaliana Juni 11, mwaka huu kati ya DPP na mshtakiwa. Alidai mshtakiwa alikiri kosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na anadaiwa kati ya Novemba 29, mwaka 2013 na Januari 23, mwaka 2014 maeneo ya Benki ya Stanbic Kinondoni na Benki ya Mkombozi Tawi la St Joseph wilayani Ilala kwa udanganyifu alijipatia Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh. 309,461,300,158.27.

Wankyo alidai katika mkataba mshtakiwa amekubali kulipa fidia ya Sh. 26,946,487,420.80 na alishalipa Sh. milioni 200.

Pia mshtakiwa amekubali kuweka dhamana mtambo wa IPTL uliopo eneo la Salasala Block D kiwanja namba 292. Wakili wa Serikali Mwandamizi, Renatus Mkude katika maelezo ya awali alidai kwamba katika akaunti ya Escrow iliyokuwapo Benki Kuu ya Tanzania, kulikuwa na fedha kwa ajili ya malipo ya umeme.

Mshtakiwa aliandika maombi BoT ya kuhamisha Dola za Marekani milioni 22 na Sh. bilioni 309 kwenda katika akaunti mbili tofauti zilizopo Stanbic benki. BoT ilihamisha fedha hizo ambazo katika uchunguzi zilitakiwa kulipiwa kodi TRA jumla ya Sh. 26,946,487,420.80.

Wakili wa utetezi, Melchisedek Lutema alidai huo ndio ukweli na ndio msimamo wa pande zote mbili.

Juni 2017, Seth katika kesi hiyo alishtakiwa pamoja na mfanyabiashara, James Rugemalira na wakili Makandege Rugemalira, ambaye ni Mkurugenzi wa VIP na mmiliki mwenza wa zamani wa IPTL na Seth ambaye ni Mwenyekiti Mtendaji wa PAP, wakidaiwa kutenda makosa hayo katika Jiji la Dar es Salaam na nchi za Afrika Kusini, Kenya na India.


GSP AUCTION MART

P.o.Box 31088 Dar es Salaam
Tanzania, Tel: + 255 687 638679 +255 654 922892
Sinza Africasana near by sokoni Africasana Block No. 31
Email: gsp.recovering@gmail.com / gsp.recovering@outlook.com

**KUMB No. AFCL/2021/DM/022**

**GSP AUCTION MART** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na kampuni ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED S.L.P 40780 Dar es salaam** tunapenda kutangaza mnada wa hadhara wa kuuza Magari kwa njia ya mnada wa magari twaja hapo chini.Siku ya Jumanne tarehe 29/06/2021 mnada utaanza Saa 5:00 kamili asubuhi katika yadi ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** iliyopo Dar es salaam vingunguti na Mwanza Sinai Mabatini.

| CUSTOMER NAME | MODEL | VEH_NO | LOCATION |
|---|---|---|---|
| MOSES PETER ABDONI | LP 909 BUS | T877 DNN | DAR ES SALAAM |
| ABDALLAH KIBWANA KIBWANA | LP 909 BUS | T351 DPS | MWANZA |
| BASHIR LEONI MSIMBE | LP 909 BUS | T163 DNT | DAR ES SALAAM |
| BASHIR LEONI MSIMBE | LP 909 BUS | T164 DNT | DAR ES SALAAM |
| LUKE ASSOCIATE LTD | PRIMA 2523 | T678 DNE | DAR ES SALAAM |
| LUKE ASSOCIATE LTD | PRIMA 2523 | T613 DMQ | DAR ES SALAAM |
| SHABAN RAJABU SOUD | LP 909 BUS | T615 DQF | DAR ES SALAAM |

1. Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.
5. Kwa yeyote atakayeharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

216313801

**KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:**
**GSP AUCTION MART PO BOX 310088 DAE ES SALAAM.**
**+255 654 922 892, +255 687 638 679**




Mwanafunzi wa darasa la tatu wa Shule ya Genesis, Markus Mmbaga, akionyesha roboti alilotengeneza, katika siku maalum iitwayo Maonyesho ya Mradi wa Sayansi, shuleni hapo, eneo la Masaki, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mke, mume wajilipua kwa petroli

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Kijiji cha Busongo, Kishapu mkoani Shinyanga, Wencheslaus James (30) na aliyekuwa mke wake Bertha Kasimili (25) wamefariki dunia baada ya kujilipua kwa petroli.

Vifo hivyo vimetokea kutokana na madai kwamba James alisikia kuwa mke wake huyo alikuwa na mipango ya kuolewa na mwanamume mwingine baada ya wazazi wake kuvunja ndoa yake.

Kutokana na kuvunjwa kwa ndoa hiyo, inadaiwa kuwa mwanamke huyo alipata mwanamume mwingine wa kumuoa na ndipo James alipopata wivu na kuamua kutekeleza unyama huo.

Kabla ya kujilipua, James alimchoma kisu cha ubavuni Bertha na kisha kumfunga na mnyonyoro pamoja na yeye na kisha kujilipua kwa petroli.

Tukio hilo lilitokea Juni 14, mwaka huu majira ya saa 4:00 asubuhi, katika kijiji cha Busongo nyumbani kwa mwanamke.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Jackson Mwakagonda, alithibitisha hayo jana alipotoa taarifa kwa vyombo vya habari na kubainisha kuwa chanzo cha tukio hilo ni wivu wa kimapenzi.

Alisema wanandoa hao walikuwa wamezaa watoto watatu, lakini wazazi wa mwanamume walimkataa mke wake na kuamua kuvunja ndoa hiyo kurudisha mahari alizotoa baada ya ndoa hiyo kuvunjika.

Mwakagonda alisema siku chache baadaye mwanamume alisikia kuwa mke wake anataka kuolewa na mtu mwingine kitendo ambacho kilimfanya kwenda kwao mwanamke akiwa na kidumu cha petroli lita tano. Baada ya kufika, alisema aliingia chumbani kwa mwanamke na kufunga mlango na kuanza kugombana.

"Mwanaume huyu alimchoma kisu cha ubavuni mke wake na kisha kumfunga minyororo na kumwagia mafuta ya petroli kisha na yeye kujifunga minyororo na kujimwagia mafuta hayo na kawasha kiberiti na kujilipua moto ambapo waliteketea wote pamoja na nyumba," alisema Mwakagonda.

# Mbunge aonya vyombo binafsi kunyimwa matangazo ya serikali

**Na Romana Mallya,** DODOMA

MBUNGE wa Gairo, Ahmed Shabiby, ameitaka serikali isiwabague wananchi wake na kutolea mfano namna vyombo vya habari binafsi vinavyonyimwa matangazo.

Shabiby alisema kama serikali inataka kufanya kila kitu, basi isamehe kodi.

Aliyasema hayo juzi jioni bungeni wakati akichangia mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22, na kueleza kwa sasa wakienda vyombo binafsi wanakuta havipewi matangazo badala yake vinapewa vya serikali ambavyo hawasomi kwa sababu wanajisifia wenyewe kwa wenyewe.

"Unakuta halmashauri inatoa tangazo inataka mkandarasi inatoa kwenye magazeti sita hajapatikana, lakini wakitoa kwenye chombo chochote cha binafsi utakuta makandarasi 80 au 40... kwa hiyo mnakula fedha zetu za halmashauri bila sababu kwa kulazimisha vyombo vya serikali lazima vifanye matangazo," alisema.

Mbunge huyo alisema pia tatizo hilo lipo kwa makandarasi, na kutolewa mfano jimbo lake la Gairo hakuna mhandisi wa wilaya bali wapo fundi mchundo.

"Hawa mafundi mchundo mnawaambia wajenge hospitali ya wilaya ikibomoka mnatumia force account yote uku mkandarasi asipate fedha kwa wakati," alisema.

Alisema serikali inataka kodi kutoka kwa watu binafsi ambao wanaajiri watu wengi, lakini hawataki wapewe kazi.

"Ukienda bandarini kuna Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) hawataki kampuni za clearing and forwarding wafanye kazi... anaingilia sheria ambazo siyo zake, iliundwa ifanye kazi ya sheria kwa sababu ya mizigo ya serikali na dawa, lakini wanaingia wafanye kazi wao," alisema.

Mbunge wa Sumbawanga (CCM), Aeshi Hillaly aliibua suala la watu wanaotengeneza Luku na kuwauzia TANESCO na baadaye hutengeneza Sub meter ambapo huwauzia wawekezaji wanaojenga nyumba za kupangisha.

"Wao wananunua kwa Sh. 380 kwa uniti na wanauza kwa Sh. 500 kwa uniti moja, je, serikali imeruhusu kuuza umeme unaozalishwa na TANESCO? Ninachojua mfanyabiashara anaweza kuzalisha umeme akaiuzia TANESCO kisha shirika likawauzia wananchi.

"Zimeibuka kampuni nyingi kwa bahati mbaya kampuni hiyo hiyo inatengeneza tokeni inauza bila serikali kujua, kodi anamlipa nani? Waziri jambo hili liangalie, watu wa TANESCO wanafahamu na ndiyo biashara yao, niite Waziri niwaeleze kwa sababu jambo hili limekuwa nikilifuatilia sana miaka mitano."



# Utouh, Prof. Ngowi: Tuwe makini na Luku, Deni Taifa, upendeleo viwanda

## ■Kujipanga mapema biashara na majirani

**Na Waandishi Wetu**

TAASISI ya WAJIBU imechambua mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, ikibainisha hoja muhimu na kutoa mapendekezo yake kwa serikali.

Uwasilishwaji wa uchambuzi huo ulifanywa jana mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo, Ludovick Utouh, akishirikiana na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Tawi la Dar es Salaam, Profesa wa Uchumi, Honest Ngowi.

Maeneo yaliyomulikwa na wataalamu hao ni pamoja na mwenendo wa Deni la Taifa, vyanzo vipya vya mapato, udhibiti wa matumizi ya mapato, mkakati wa serikali kulinda viwanda vya ndani na athari zake, kodi ya biashara za mtandaoni na vikwazo ambavyo wanafikiri vitaibuka katika utekelezaji wa bajeti hiyo ya kwanza chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Utouh ambaye aliwahi kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka minane kuanzia mwaka 2006, alisema uchambuzi wao umebaini bajeti hiyo imeweka malengo ya jumla yanayojumuisha kuboresha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji kodi ili kupanua wigo wa kodi.

Alisema malengo mengine ni kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara, kuimarisha uendeshaji wa mashirika ya umma ili yafanye kazi kibiashara, kuongeza uzalishaji wa mazao ya sekta za mifugo, kilimo na uvuvi, na kuchochea uwekezaji hasa katika viwanda vinavyotumia malighafi za ndani.

Utouh aliyataja malengo mengine kuwa ni kupambana na utoroshaji wa madini na kujenga mitambo ya uchenjuaji wa madini nchini, kuboresha miundombinu ya sekta za usafirishaji na nishati, kuboresha utoaji wa huduma za kijamii katika sekta za afya, elimu na maji pamoja na kuimarisha uhusiano wa kimataifa.

Profesa Ngowi, akimulika mikakati ya kudhibiti matumizi, alisema bajeti hiyo inalenga kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi na kuhakikisha miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya kuanzisha miradi mipya.

Alisema mkakati mwingine uliowekwa kwenye bajeti hiyo ni kudhibiti uzalishaji na ulimbikizaji wa madeni, kuendeleza nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na kuongeza matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa fedha za umma.




Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Tawi la Dar es Salaam, Profesa Honest Ngowi, akichambua bajeti inayopendekezwa na serikali kwa mwaka ujao wa fedha mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, Ludovick Utouh.

"Bajeti ina viashiria vya kusaidia kukuza uchumi kwa kuhusianisha uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji. Serikali imeonyesha lengo la kulinda viwanda vya ndani kwa kupunguza ushindani wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi kwa kupunguza kodi kwa baadhi ya malighafi zinazotoka ndani ya nchi.

"Bajeti inaashiria kuboresha hali ya uchumi kwa jamii kwa kuongeza wigo wa kipato kinachotokana na mshahara kwa kupunguza kiwango cha wastani wa PAYE (Kodi ya Lipa Kadri Unavyopata) kutoka asilimia tisa (9) hadi nane (8).

"Bajeti inaonyesha eneo la kujenga jamii yenye uwezo wa kushindana kikanda na kimataifa limetengewa kiasi cha Sh. trilioni 7.44, miradi ya kielelezo imetengewa Sh. trilioni 3.13 na miradi mingine imetengewa Sh. trilioni 4.31," Prof. Ngowi alisema.

**VIKWAZO**

Katika uchambuzi wao, wamebaini utekelezaji bajeti pendekezwa huenda ukakumbwa na vikwazo kadhaa vinavyojumuisha mkakati wa serikali katika kulinda viwanda vya ndani kupitia kupunguza vikwazo vya kodi.

Profesa Ngowi alisema pamoja na nia njema ya serikali kulinda viwanda vya ndani, hatua hiyo inaweza kuwadhuru walaji kwa kuwapunguzia uhuru wa uchaguzi wa bidhaa kuendana na thamani na ubora wa bidhaa katika soko.

Alisema kikwazo kingine ni kuendelea kupanda kwa bei ya mafuta kunakotokana na ugonjwa wa corona duniani huenda kutaongeza bili ya uagizaji wa mafuta kutoka nje ya nchi.

Mtaalamu huyo wa uchumi alisema kuna hatari serikali kukosa fedha za kulipa madeni kutokana na utaratibu unaoendelea wa kukopa ili kutekeleza miradi mikubwa.

Alisema kikwazo kingine wanachokiona ni ufanisi duni katika matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa matumizi.

**DENI LA TAIFA**

Ili kukabiliana na kasi ya kuongezeka kwa Deni la Taifa, Utouh alisema wanaishauri serikali kuongeza vyanzo vipya vya mapato, kuboresha uhusiano na nchi wahisani ili kupata misaada ya kugharamia bajeti ya nchi na serikali ikope mikopo yenye riba nafuu na kuachana na mikopo ya masharti ya kibiashara.

**KODI KWA LUKU**

Kuhusu kodi ya pango kulipwa kupitia ununuzi wa umeme kupitia Luku, Utouh alisema ni wazo zuri lakini kuna haja serikali kuweka mfumo mbadala wa kusaidia pale mfumo mkuu utakaposhindwa kufanya kazi huku wakitaka kutazama kwa undani tozo hiyo kulipwa na wapangaji badala ya mmiliki wa nyumba, nyumba maalum za makazi ya wazee na nyumba za makuti ambazo hazipaswi kulipiwa tozo hiyo.

"WAJIBU pia inaona umuhimu wa kufanyia marekebisho Sheria ya PPP ya Mwaka 2010 ili kufanikisha utekeleza wa bajeti pendekezwa.

"Mfano, anayegharamia upembuzi yakinifu analazimika kuingia kwenye ushindani ili kutekeleza mradi. Hii inahatarisha uwekezaji wa kwanza endapo aliyegharamia upembuzi yakinifu atashindwa kupata zabuni hiyo," Utouh alifafanua.

**RIPOTI ZIWEKWE WAZI**

Utouh alisema ripoti zote za utendaji wa taasisi za udhibiti nchini (mfano TAKUKURU, Msajili wa Hazina na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma) ziwe zinawasilishwa bungeni ili kujadiliwa na kufanywa kuwa taarifa za wazi kwa wananchi.

"Ripoti zinazotolewa na CAG kwa maofisa masuuli, bodi za wakurugenzi na bodi za ushauri za taasisi za serikali (management letters) ambazo sasa ni siri ziwe wazi kwa umma.

"Ikumbukwe kuwa watumishi wa umma wanasimamia tu rasilimali za umma kwa niaba ya wananchi ambao ndiyo wamiliki wa rasilimali hizo, hivyo wana haki ya kufahamu udhaifu uliobainishwa na CAG katika usimamizi wa rasilimali zao," alisema.

**BIASHARA MTANDAONI**

Mtaalamu huyo wa masuala ya fedha alisema serikali kupitia TRA na BoT na TCRA, ifanye uwekezaji mkubwa katika kujenga uwezo wa kutambua na kutoza kodi biashara zinazofanyika kupitia mtandao ambazo zinakua kwa kasi kubwa nchini.

Utouh pia alilishauri Bunge kupitia Kamati yake ya Bajeti kufanya usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa bajeti itakayoidhinishwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa kuhakikisha linapitia ripoti za utekelezaji wa bajeti za robo mwaka zinazotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango.

**MAZUNGUMZO NCHI JIRANI**

Alisema wanaishauri serikali kuanza mazungumzo ya kuuziana bidhaa na huduma za ziada zinazotokana na miradi ya kimkakati, mfano umeme na usafirishaji wa mizigo kupitia reli ya kisasa (SGR).

Utouh alisema hatua hiyo itasaidia kuihakikishia serikali kuwa na fedha za kigeni za kuhudumia madeni yanayotokana na miradi hiyo pindi yatakapoanza kulipwa.

"Serikali ihakikishe inaziongeza uwezo wa kifedha, watumishi na miundombinu mahakama za usuluhishi wa kodi ili ziweze kusikiliza na kuamua mashauri ya kodi ambapo hivi sasa kuna Sh. trilioni 360.08 na Dola za Marekani milioni 181.43 viporo vya kufanyiwa uamuzi ili serikali ipate mapato stahiki kutoka katika mashauri hayo," alisema.

Utouh pia alisema serikali inapaswa kupunguza idadi ya miradi inayopangwa kutekelezwa kwa mwaka ili kuipa nafasi kutenga kiasi kikubwa zaidi katika kutekeleza miradi michache ambayo itakamilika kwa wakati.

"Tunaipongeza serikali kupunguza muda wa miaka 12 hadi sita (6) kwa watumishi wa Jeshi la Polisi kupata mafao yatokanayo na utumishi wao.

"Hata hivyo, WAJIBU tunaishauri serikali kuondoa kabisa muda wa miaka sita kwa watumishi wa jeshi hilo ili kuwapa haki ya kupata mafao ya utumishi wao.

"Kwa ujumla, tunaipongeza serikali kwa kukamilisha uandaaji wa bajeti ya mwaka 2021/22 pamoja na kubuni vyanzo vipya vya mapato, mfano kodi ya laini za simu, hati fungani za manispaa pamoja na tozo ya pango kupitia Luku za umeme," Utouh alihitimisha.

Katika bajeti hiyo, serikali inapendekeza kutumia Sh. trilioni 36.329, kati yake, asilimia 63 inaelekezwa kwa matumizi ya kawaida na asilimia 37 kwa ajili ya maendeleo kama ilivyokuwa mwaka huu wa fedha.

HABARI KITAIFA

# Samia, Mpango watoa neno Siku ya Mtoto wa Afrika

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewataka wazazi na jamii kwa ujumla kutafakari ni kwa kiwango gani wanatetea haki za watoto na wajibu wa malezi sahihi.

Katika ukurasa wake wa twitter aliandika "Tunapoadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika nawasihi wazazi wenzangu na jamii kwa ujumla kutafakari ni kwa kiwango gani tunatetea haki za mtoto, tunawalinda dhidi ya unyanyasaji, ukatili na tunatimiza wajibu wa kuwapa malezi bora na furaha. Nawatakia kheri watoto wote wa Afrika."

**MAKAMU WA RAIS**

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza wakati wa uzinduzi wa Makao ya Taifa ya Watoto, yaliyopo Kikombo jijini Dodoma, alitoa maagizo sita kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ikiwamo kudhibiti uanzishaji holela wa makao ya watoto bila kuwa na vibali kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo, alishauri wizara hiyo kupitia upya masharti na taratibu za kuasili watoto ili kuhamasisha Watanzania na wenye nia njema kuasili watoto ili kupunguza idadi yao kwenye makao.

Alizitaka wizara hizo kuhakikisha makao yanayoanzishwa yanakuwa na leseni na walezi wa kutosha na wenye sifa stahiki na utoaji wa huduma zinazozingatia taratibu za kiafya.

"Hakikisheni mnasimamia na kuhakikisha kuwa watoto wanalelewa kwa kuzingatia mila, tamaduni na desturi za kitanzania," alisema.

Aidha, alizitaka wizara za TAMISEMI na Afya kuhakikisha zinaweka mfumo wa kuhakikisha misaada inayotolewa na wasamaria wema kwenye vituo vya kulea watoto yatima na wasiojiweza inawafikia walengwa.

"Shirikianeni kusimamia na kuhakikisha kuwa huduma katika makao ya watoto zinazotolewa kwa kuzingatia kiwango, matakwa ya sheria na kanuni husika, pia wekezi maandalizi ya wototo kurejea katika jamii kama vile kuwachanganya na wenzao katika maeneo mbalimbali kama vile shuleni, vyuo vya ufundi," alisema.

Awali, Waziri wa Afya, Dk. Dorothy Gwajima, alisema kama sehemu ya maadhimisho hayo serikali imezindua makao ya watoto na kuitaka jamii kufanya tathmini sababu za ongezeko la watoto wa mitaani.

Alisema ujenzi wa makao hayo unatarajia kuwezesha serikali kutatua tatizo la Makao ya watoto kwa kuwa kituo cha Kurasini ni kidogo, na kwamba ujenzi umegharimu Dola za Kimarekani milioni 5.5 sawa Sh. bilioni 12.7 na kuna watoto 28.

**TAMWA YAKUTANA NA WATOTO**

Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), kimeadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika, kwa kuwakutanisha pamoja watoto kutoka sehemu mbalimbali za Dar es Salaam, kwa lengo la kuwapa elimu ya kutambua haki zao na aina za ukatili wa kijinsia.

Mafunzo hayo yaliyoambatana na michezo, yalilenga kuwajengea uwezo wa kujitambua na kutoa taarifa za matukio ya ukatili wanaoyokutana nayo kwa lengo la kuyatokomeza nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Rose Reuben, akizungumza katika tamasha hilo la kuadhimisha siku hiyo lililofanyika katika ofisi zao jijini Dar es Salaam jana, alisema pia wamewapa elimu ya wapi waripoti matukio ya ukatili.

"TAMWA katika kuadhimisha siku hii tunapata nafasi ya kucheza na kufurahi na watoto. Lakini tunatoa elimu ya haki za watoto, wazifahamu, wajue ina za ukatili wanaotendewa na watu wanaowafahamu na wasiyo wafahamu ili watoe taarifa," alisema Rose.

Alifafanua zaidi kuwa sababu ya kutoa elimu ya kutambua matukio hayo inatokana na takwimu za Jeshi la Polisi, zinazoonyesha matukio ya ukatili yameongezeka kwa asilimia 26 kutoka mwaka 2015 hadi mwaka 2020.

Alisema mwaka jana yaliripotiwa matukio 7,263 wakati mwaka 2015 yaliripotiwa matukio 5,803 ikiwa ni ongezeko la matukio 615 kwa mwezi na kusema kuwa linahatarisha mustakabali wa watoto nchini.

**PICHA MTANDAONI**

Naye Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Maendeleo ya Mtoto katika Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wazee na Watoto, Sebastian Kitiku, alisema serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), watakutana na kampuni za simu za mkononi kuweka mfumo ambao utafuta picha zisizo na maadili zinazochangia matukio ya ukatili kwa watoto.

Aidha, alisema Mkoa wa Tanga unaoongoza kwa matukio ya ukatili dhidi ya watoto ukifuatiwa na Mbeya, Mwanza, Dodoma na Kilimanjaro na kwamba mikoa hiyo inatazamwa kama kipaumbele katika kutoa elimu, ili kukabiliana na matukio hayo.

Alisema simu za kisasa za mkononi ambazo wazazi huwapatia watoto wao na kuzitumia kumeongeza matukio ya ukatili kwa kurubuniwa ikiwamo ubakaji.

"Tunafikiria kukutana na kampuni za simu za mkononi kupitia TCRA, tukutane, wao wana mfumo ambao unaweza kuondoa picha isiendelee kusambaa mtandaoni, watoto wasizipate. Mfumo huu utasaidia kuwalinda watoto kwa kuziondoa picha hizo, ambazo kisheria haziruhusiwi.

"Unapomkabidhi mtoto wako simu ya 'smartphone', unachangia siku zote kuharibikiwa, ukimpa simu hakikisha anatumia simu mbele yako, usimpe akaingia nayo chumbani, atajiingiza kwenye matatizo makubwa yatakayomwathiri, mara nyingi anaweza akarubuniwa kingono kwenye mitandao ya kijamii.

"Kuna wazazi wengine wanadiriki hata kumnunulia mtoto simu sababu amefaulu vizuri, watoto wetu wamezaliwa katika dunia ya kidigitali, wanajua zaidi, wanatazama picha zisizo na maadili kupitia simu za wazazi. Hatua za haraka zichukuliwe kunusuru watoto wetu," anasema Kitiku.

Aidha, Kitiku alisema takwimu za mwaka jana za Jeshi la Polisi zinaonyesha yalikuwapo matukio 5,700 huku kati yake yakiongoza ya ubakaji.

Siku ya Mtoto wa Afrika, huadhimishwa kukumbuka tukio la mauaji ya watoto ambao walikuwa wanafunzi mjini Soweto, nchini Afrika Kusini Juni 16, mwaka 1976 na Umoja wa Mataifa (UN), kuitambulisha kuwa siku ya kimataifa.


Akiba Commercial Bank yapata Mkurugenzi Mtendaji Mpya

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
benki kwa maendeleo yako



Mr. Silvest Arumasi

Benki ya Biashara ya Akiba (Akiba Commercial Bank) imeingia ubia na Benki ya Taifa ya Malawi (National Bank of Malawi) kama mkakati wa kujiimarisha na kutoa huduma bora kwa wateja.

Hivyo Bodi mpya ya Wakurugenzi wa Benki hiyo imemteua Bw. Silvest Arumasi kuwa Mkurugenzi Mtendaji mpya kuanzia mwezi Juni, 2021.

Bwana Arumasi ni Mtanzania ambae kitaaluma ni mhasibu, ana uzoefu wa kibenki wa miaka 17 ikiwemo miaka 7 katika Benki Kuu ya Tanzania (BOT) na pia katika Benki za First National Bank (FNB) na Benki ya Biashara ya Taifa (NBC) katika nyadhifa za uongozi wa juu.

Mwenyekiti mkongwe wa Bodi ya Akiba, Bw. Ernest S. Massawe ambaye ataendelea kuongoza Bodi hiyo mpya ameelezea furaha yake ya kumpata Mtendaji Mkuu mpya atakaye ifikisha benki kwenye sura ya mafanikio zaidi miaka ijayo. Benki ya Akiba yenye jumla ya matawi 18 Dar es Salaam, Arusha, Moshi, Dodoma, Mwanza na Mbeya ilianzishwa mwaka 1997 na Watanzania takribani 300 waliovutiwa na sera mpya ya ubinafsishaji kwenye sekta ya fedha na Imani yao kwamba mamilioni ya wajasiriamali wadogo na wa kati wangeweza kujiendeleza na kuboresha maisha yao kwa kupata huduma za kibenki kwenye benki yao.

Benki itaendeleza sera ya msingi ya muda mrefu ya kutoa huduma kwa wateja wadogo, wakati na pia wakubwa na kueneza huduma kote nchini hatua kwa hatua.

Dora Saria

Mkuu wa kitengo cha Masoko na Mawasiliano
Akiba Commercial Bank Plc

216309201

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utoaji Vitambulisho vya Taifa usimamiwe vyema

**JUZI** serikali ililieleza Bunge kuwa kupitia mpango kazi wa kuzalisha vitambulisho, inatarajiwa kuwa ifikapo Agosti, mwaka huu, wananchi wote waliotambuliwa na kupewa namba za usajili watakuwa wametapatiwa vitambulisho vyao.

Hakikisho hilo lilitolewa bungeni na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Martha Mariki.

Alisema kwa kipindi cha miezi mitano (Januari 14- Mei 13, 2021), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imezalisha na kusambaza vitambulisho 7,148,971 katika wilaya 73.

Aidha, hadi kufikia mwezi Mei, 2021, Mamlaka imegawa namba za utambulisho (NIN) kwa wananchi zaidi ya milioni 11 kutokana na mfumo wa NIDA kuunganishwa na mifumo mingine ya taasisi za serikali na binafsi.

Hii ni habari njema kwa mamilioni ya wananchi ambao kwa muda mrefu wana namba, lakini hawajapata vitambulisho viwasaidie kama inavyotakiwa.

Mara kadhaa serikali imekuja na ahadi za kuboresha utoaji wa vitambulisho hivyo na ya kwanza ni mwaka 2015, ambayo kila aliyekuwa na kitambulisho cha zamani alitakiwa kurudisha na kupewa kipya, ambacho kina saini yake.

Hata hivyo, baadaye kulikuwa na kusuasua kupatikana kwa vitambulisho hivyo na kasi iliongezeka wakati wa usajili wa laini za simu kwa kutumia alama za vidole, lakini wengi waliishia kupata namba.

Januari mwaka huu, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alisema mwishoni mwa mwezi huo, wangeanza kuchapisha vitambulisho 144,000 kwa siku.

Alisema NIDA itafanyakazi saa nane mchana na saa nane usiku jumla 16, na kwamba kwa mashine mpya inaweza kuzalisha vitambulisho hivyo ili kuhakikisha kila Mtanzania anapata kitambulisho hicho.

Ahadi ni kuwa hadi mwishoni mwa mwaka huu, kila Mtanzania atakuwa na kitambulisho cha Taifa, huku sababu inayotolewa ni kuwa mtambo uliokuwapo ulikuwa unazalisha vitambulisho vichache na sasa kupitia mtambo mpya, uzalishaji utaongezeka maradufu.

Hii ni ahadi ya pili yenye matumaini makubwa kwa Watanzania walio na namba bila vitambulisho, hivyo tunaamini sasa kutakuwa na usimamizi wa karibu kuhakikisha inatimia.

Huku nyuma kulikuwa na sababu nyingi zilizotolewa kiasi cha kukwamisha upatikanaji wa vitambulisho hivyo, hali iliyowafanya wengi kukata tamaa kufuatilia, na wengine wakifika kwenye ofisi za NIDA maeneo yao bila mafanikio.


Matarajio ya Watanzania ni kuondokana na kero hiyo na sasa vitambulisho kupatikana kama inavyotakiwa ili viwasaidie katika huduma ambazo huhitaji vitambulisho vya utaifa.

Aidha, tunaishauri serikali kufuatilia kwa kina madai ya uwapo wa vitambulisho bandia ambavyo vinatumika katika maeneo yanayohitaji vitambulisho, jambo ambalo litasababisha matatizo makubwa na baadhi ya watu wanadaiwa kutapeliwa kwa kutumia vitambulisho bandia.

Pia ni muhimu malengo ya kuwa na vitambulisho hivyo yakasalia kama ilivyokuwa awali, kwa kuwa tulihakikishiwa sasa tutaachana na kuwa na vitambulisho vingi bali vya NIDA, ambavyo vitatumbulisha mtandaoni kiasi kwamba hakuna haja ya kutoa nyaraka hiyo kila mahali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# 'Kuchimba dawa' porini si haki kwa mama, mazingira

**'KUCHIMBA** dawa' sio msamiati mgeni kwa mtu anayesafiri walau safari ndefu, kutoka mkoa mmoja kwenda nyingine, japo si neno rasmi. Inaendana na haja ya kibinadamu kujisitiri kiafya. Hapo ndipo kunakozaa msamiati ulioundwa.

Namna inavyokuwa, ni kwamba mtu anapopanga safari kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine hasa safari ya mbali, huwa tunawasikia makondakta wa mabasi wanawaambia abiria kupitia tamko "umefika muda wa kuchimba dawa" na dakika zinazotajwa jumla yake ni tano. Hilo la 'kuchimba dawa' mara nyingi tumekuwa tukiona gari zinaingia katika hoteli na abiria wanachuka na kwenda katika maeneo ya huduma za kuchimba dawa ndani ya migahawa husika na abiria wengine wakitumia dakika hizo kadhaa kujisitiri dhidi ya njaa na kiu, wakinywa chai.

Kinamama nao hawako nyuma. Ndio wakati wa kuwabadilishia watoto pampasi na mambo yanayofanana nayo.

Nirejee mfano wa abiria anayesafiri kutoka jijini Dar es Salaam, mathalan kwa safari ndefu kama vile kwenda jijini Mwanza. Hapo gari linatangaza watu kuchimba dawa katika maeneo matatu, tena inakuwa katika huduma za hoteli au migahawa iliyoko njiani.

Lakini, kuna sura ya pili kwa binadamu anabaki kuwa binadamu, huku wakitofautiana katika hulka na maumbile yake kiafya.

Cha kushangaza ni kwamba, kwa sasa kumetokea tabia mabasi yanagoma kuruhusu abiria kuchimba dawa katika maeneo ya porini, kwa madai wanaweza kupigwa faini.

Unakuta abiria analalamika aweze kuchimba dawa, lakini wanakataa kumsaidia na kumwambia avumilie mpaka afike sehemu ya walikopanga, huku baadhi ya mabasi yakirejesha hilo linafanyika porini.

Kinachosikitisha ni kwamba namna 'uchimbaji dawa' unavyofanywa na baadhi ya mabasi hayo, uko katika sura ya kumdhalilisha mwanamke.

Niweke sawa kwamba, ninapotamka hilo la kumdhalilisha mwanamke, ninamaanisha tendo hilo linafanyika katika namna inayomfanya mwanamama huyo asidhalilike katika safari hiyo vichakani.

Unakuta basi linalobeba abiria zaidi ya 60 au 50, linaegeshwa mahali pori kwa dakika tano tu. Hapo unajiuliza, sehemu yenyewe porini na abiria wa kike wanaweza vipi kutumia muda huo, wawe wamemaliza kuchimba hiyo dawa?

Mbaya zaidi katika kushindana na muda huo wa kujifariji, mwanamama anashindwa kwenda mbali, bali anachimba dawa anaonekana. Hii maana yake nini, kiutu na mustakabali mpana wa dhana hiyo? Kitendo cha 'kuchimba dawa' porini linabeba udhalilishaji wa mwanamke, hivyo waendeshaji na wahudumu wa magari hayo, wanapaswa kujenga mazingira ya 'kuchimba dawa' kwenye migahawa au sehemu zinazofanana nazo. Hapo ataweza kujistiri vizuri.

Mwanamke ana haki zake na asidhakikiwe kupitia 'uchimbaji dawa' wa aina hiyo. Anapaswa kulindiwa heshima stahiki na njia bora ni mabasi yapelekwe hotelini na kamwe sio porini.

Inanishangaza kwamba, katika baadhi ya mabasi huwa wanapaki magari pembezoni mwa barabara, wakiwalekeza abiria wakajisitiri.

Sasa kupaki gari pembezoni mwa barabara na mnawaambia abiria washuke maeneo hayo 'wakachimbe dawa' penye uwazi huo, sheria na haki zao ziko wapi?

Tukumbuke kuwa kuna tofauti kubwa kati ya mwanamke na mwanaume kijinsia na maumbile. Ukweli ni kwamba, mwanaume anaweza kusimama kokote kujisitiri, lakini mwanamke anatakiwa kujificha kuchimba dawa tena mbali na aliko mwanaume.

Kwa kufanya hivyo, wenye mabasi mnawadhalilisha sana wanawake 'kuwachimbisha dawa' hadharani.

Mnapoanza safari, huwa mnaingia katika hoteli zenu mnatoa dakika 10 za kuchimba dawa na mnajua hapo abiria watanunua ya vyakula na chai, pia vitafunwa, kila mmoja akijisitiri mlo kwa namna yake.

Awamu ya pili, inakuwa pale wanawaingiza abiria 'kuchimba dawa' katika migahawa inayowahusu. Hapo inatengwa dakika 10, wakipewa na fursa kwenda kuhudumiwa vyakula mgahawani.

Sasa kama mnajua tofauti hiyo ya muda na mazingira, inakuwaje safari inaopoendelea, sasa 'kuchimba dawa' awamu ya tatu, abiria wanapelekwa kandi ya baabara tena kwa udhalilishaji uleule wa kinamama, wakirejea dakika tano zilezile?

Pia, hapo kuna tafsiri nyingine ya faragha hiyo ya 'kuchimba dawa' kwamba inaangukia kumdhalilisha mwanamke. Kama ndiyo hivyo, suluhisho lake nini? Ni busara kwamba, ikiwa 'uchimbaji dawa' unaelekezwa hotelini, uendelee hivyo hivyo hadi mwisho wa safari na si vinginevyo, kurejea porini.

# TANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MARUDIO:

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA YA KUJENGA NYUMBA MBADALA KWA AJILI YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) KUMBUKUMBU NA: 0010006840

TOTAL East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, kampuni ya Mafuta na Gesi, inaalika makampuni yenye uzoefu na sifa kutuma nia ya kujenga nyumba mbadala kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha Mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni karibia kilomita 1,443, kati hizo kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Katika upande wa Tanzania bomba litapita katika mikoa nane (8), halmashauri za wilaya 27 na vijiji 231.

### MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:

Ujenzi wa nyumba mbadala na majengo tegemezi (jiko na vyoo) kwa Waguswa wa Mradi (PAPs) wanaohamishwa na Mradi wa Bomba utafanyika katika mikoa nane tofauti; Kagera, Tabora, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Manyara na Dodoma.

Mradi utajenga nyumba mbadala katika ardhi iliyokubalika kwa waguswa stahiki wanaohamishwa makazi. Mradi utabainisha aina za muundo wa majengo mbadala yatakayojengwana maeneo kwa makubaliano na kila Mguswa wa Mradi. Mkadarasi atajenga nyumba 336, Vyoo vilivyoboreshwa vyenye mfumo wa kuzungusha hewa 388 na majiko ya nje 345 kutokana na michoro iliyosanifiwa kwa kina na Kampuni ambayo yote imeandaliwa kwa viwango vya usawa vya ujenzi wa nyumba.

Muundo wa chini na juu (msingi uliofungwa nondo na kumwagiwa zege, kuta za ndani/nje) kwa kila nyumba pamoja na nyumba tegemezi zitajengwa kwa kutumia vifaa vya vipimo vitakavyotolewa na Kampuni na vinavyoweza kutumika zaidi ya mara moja na kwa kutumia mseto wa zege uliosanifiwa kwa kazi husika.

Wakandarasi wote watategemewa kufanya kazi kwa kutumia mfumo huu wa vifaa vya vipimo vitakavyotolewa. Ukamilishaji wa kazi yote inayobakia (vibarua na rasilimali) kama vile kupaua, kukamilisha ujenzi, umeme na miundo mbinu ya maji safi na maji taka, kazi za ujenzi na uboreshaji wa muonekano wa ardhi zitakuwa ni jukumu la Mkandarasi.

Wazabuni watakao kidhi vigezo vya awali watapokea taarifa za muundo wa vifaa vyenye vipimo vitakavyoonyesha wazi na kuwa na taarifa za kina juu ya utengenezaji wa bidhaa husika.

Nyumba mbadala kwa ujumla zitakuwa zina kati ya vyumba viwili mpaka vitano, vyenye ukubwa wa eneo la sakafu wa mita za mraba 25 mpaka 75. Kila nyumba itakuwa na miundombinu tegemezi miwili, yaani jiko na choo cha shimo kilichoboreshwa chenye mfumo wa kuzungusha hewa. Nyumba mbadala zitakuwa za kiwango bora cha ujenzi. Kwa muundo wa chini na juu wa nyumba, nyumba zote zitajengwa kwa kutumia malighafi zinazopatikana katika maeneo husika, zote zitakidhi viwango vya ujenzi vya ubora vya Tanzania .

### VIGEZO MUHIMU:

Kutokana na ukubwa wa kazi na ili kuyasaidia makampuni yanayoonyesha nia, Mradi una haki ya kutoa kazi moja moja au pia kazi zaidi ya moja kwa mkandarasi atakayeonyesha nia na mwenye kukidhi vigezo. Kampuni zenye nia zinaweza kuingia mikataba na kampuni nyingine ili kuwezesha uwezo wao wa kutoa huduma, lakini wote kwa Pamoja na kila mbia katika mkataba ni LAZIMA akidhi matakwa tajwa yaliyoainishwa hapo chini.

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Kampuni ya Kitanzania ya Ukandarasi (Ujenzi) iliyosajiliwa kwa kiwango cha chini cha daraja la pili (wasilisha nakala),
- Mifano ya uzoefu wa kujenga majengo katika mkoa wa Kagera, Tabora, Geita, Shinyanga, Singida, Manyara na Dodoma Tanzania. (Wasilisha orodha ya miradi iliyofanyika katika mkoa wowote tajwa au mikoa yote),
- Thibitisha uwezo wa kifedha wa kutekeleza kazi tajwa,
- Thibitisha/wasilisha sera za Afya, Usalama na Mazingira (HSE/OSHA), na Usimamizi wa Viwango vya Ubora na maswala ya Jamii,
- Wasilisha/Thibitisha uzoefu wa kusimamia miradi, utaratibu wa ugavi na usafirishaji vitu Pamoja na manunuzi,
- Dhamira ya kuongeza thamani katika uwezo wa ndani/taifa (wasilisha taarifa za kina za mafunzo),
- **Uthibitisho wa usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) ya EWURA wakati wa kuwasilisha taarifa ya nia unahitajika.**

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: tolal.mufti@external.total.com (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00 jioni** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **15 Julai 2021.**

Taarifa ya kina itawasilishwa na Kampuni ili kutoa taarifa zaidi kuhusu huduma, ratiba ya utekelezaji pamoja na kutoa kipindi cha maswali na majibu kutoka kwa wazabuni wenye nia - undani wa taarifa utawasilishwa katika hatua ifuatayo.

**Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya Makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).**

# Mwili wa Prof. Baregu kuagwa leo

**Na Mwandishi Wetu**

MWILI wa aliyekuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na mwanazuoni nguli, Prof. Mwesiga Baregu, unatarajiwa kuagawa nyumbani kwake leo, Kunduchi, Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyowekwa kwenye mitandao ya kijamii na Katibu Mkuu wa CHADEMA, kiongozi na mwanazuoni huyo ataagwa kabla ya kusafirishwa kwenda mkoani Bukoba mkoani Kagera kwa maziko.

"Juni 17, mwaka huu, mwili utaletwa nyumbani Kunduchi, Juni 18 ibada na kuaga kanisani Kunduchi, Juni 19 kusafirishwa na Juni 20 mazishi Bukoba Vijijini (Maruku/Batairuka," ilibainisha taarifa hiyo.

Mwanazuoni na mwanasiasa huyo aklifariki dunia Juni 13, mwaka huu, baada ya kukaa chumba cha uangalizi maalum kwa siku 15 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Prof. Baregu atakumbukwa kama msomi aliyefanya siasa bila kuharibu kazi zake za kitaaluma na Mjumbe wa iliyokuwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba chini ya uenyekiti wa Jaji Joseph Warioba.

Alikuwa profesa wa sayansi ya siasa na utawala wa umma na profesa nguli wa masuala ya uhusiano wa kimataifa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) hadi mwaka 1998 alipostaafu kwa mujibu wa sheria.

Baada ya hapo alifanya kazi kwa mkataba hadi mwanzoni mwa miaka ya 2010 alipositishiwa mkataba wake kwa kile kilichoelezwa kuchanganya utumishi na siasa. Baadaye alijiunga na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine (SAUT).

Mbali na kuwa mwanataaluma, Prof. Baregu alikuwa mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA hadi mwaka 2019.




Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge, akikata utepe kuzindua awamu ya pili ya utengenezaji wa magari mapya ya kubebea mizigo aina ya Hong Yan, katika kiwanda cha GF, mkoani Pwani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


*Notice/Summons to appear (O.V.R.20 (1) of (CPC)*
*(Substituted Service)*

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR-ES-SALAAM**

**MISC.LAND APPLICATION NO. 247 OF 2021**

**DAR ES SALAAM WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY ..............................1ST APPLICANT**

**THE ATTORNEY GENERAL .................................... 2ND APPLICANT**

**VERSUS**

**TABU HASSAN (as a legal representatife of the late SALMA PILI TAMAA MBELE) .............................. 1ST RESPONDENT**

**MSOLOPA AUCTION MART & TRIBUNAL BROKER ......................................... 2ND RESPONDENT**

TO: MSOLOPA AUCTION MART & TRIBUNAL BROKER,
**DAR ES SALAAM.**

**WHEREAS:** The above named Plaintiffs has instituted a suit against you; you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorized on **14th** day of **July, 2021** at **09:00 am** before **Hon. Opiyo, J (1st Floor room 1)** to answer the said suit; and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your defence.

TAKE NOTICE that, in default of your appearance on that day before mentioned, the suit will be heard and determined in your absence.

Given under my Hand and the seal of this court, this 15th day of June 2021.

**DEPUTY REGISTRAR**
**HIGH COURT OF TANZANIA**
**LAND DIVISION**

216314102


# Watatu kunyongwa hadi kufa

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Kigoma imewahukumu watu watatu kunyongwa hadi kufa, baada ya kukutwa na hatia ya mauaji ya mlinzi.

Mlinzi huyo alikuwa akifanya kazi katika kampuni ya kichina iliyokuwa inatengeneza barabara ya Kasulu-Kidawe mkoani Kigoma.

Kesi hiyo namba 36 ya mwaka 2020 ilikuwa ni Jamhuri dhidi ya washtakiwa hao watatu ambao ni Nuru Venevas, Seth Simon na Ezekiel Kalobezi.

Ilielezwa mahakamani hapo kwamba tukio hilo la mauaji lilitokea Oktoba 2, 2016, miongoni mwa washtakiwa hao ni aliyekuwa dereva wa mtambo wa kutengenezea barabara katika kampuni hiyo, ambaye alipanga njama na wenzake hao wawili ili waibe kifaa kilichotajwa kwa jina la control box.

Akisoma maelezo ya kesi hiyo kabla ya kutoa hukumu, Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma, Athuman Matuma alisema upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili Robert Magige ulikuwa na mashahidi nane pamoja na vielelezo, huku upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili Aliki Saiki.

Jaji Matuma alieleza kuwa kwa mujibu wa ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri na kuwasilishwa mahakamani hapo, washtakiwa wakiwa katika harakati za wizi wa kifaa hicho walidhibitiwa na aliyekuwa mlinzi katika eneo hilo ajulikanaye kwa jina la Richard Chija.

Alieleza kuwa washtakiwa hao walimshambulia mlinzi huyo ili watimize adhima yao ya kuiba na kusababisha mlinzi huyo kupata majeraha sehemu mbalimbali za mwili wake na kusababisha kifo.

Jaji Matuma alieleza kuwa shahidi upande wa Jamhuri ambaye ni daktari aliyeufanyia uchunguzi mwili huo alieleza kuwa kifo hicho kilisababishwa na kuvuja damu nyingi baada ya kupigwa.

Jaji Matuma alisema licha ya kwamba kielelezo kilikamatwa kwa mshtakiwa namba mbili ambaye ni Seth Simon, lakini ukamataji huo uliwezeshwa na maelezo yaliyoendana baina ya washtakiwa wawili ambao mmoja aliyekuwa na kifaa hicho na mwingine alielekeza sehemu alipo mshtakiwa huyo.

Alisema baada ya kufuata taratibu za upekuzi mshtakiwa huyo alikutwa na kifaa hicho kikiwa chumbani kwa kaka yake mkoani Geita alikokuwa amekimbilia.

Jaji Matuma alieleza maelezo waliyoyatoa washtakiwa hao polisi yaliwezesha kupatikana kwa kifaa hicho ambacho kilitambuliwa kwa namba na kufanya kazi kiliporudishwa kwenye mtambo.

Alieleza japo washtakiwa waliyakataa maelezo hayo mahakamani kwa kusema waliyaandika kwa kulazimishwa na kupigwa na Jeshi la Polisi.

"Maelezo ya washtakiwa hawa watatu yanaendana na yamebeba ukweli wenye hatia wa utekelezaji wa tukio la mauaji," alisema Jaji Matuma.

Aliongeza kuwa mahakama ilijiridhisha kuwa washtakiwa wote watatu walikuwa na hatia, kila mmoja amehukumiwa kunyongwa hadi kufa.

## NMB kukopesha makandarasi bila dhamana

**Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imewaalika makandarasi wa ndani na nje wenye mikataba ya ujenzi wa miradi ya miundombinu inayotekelezwa nchini kwenda kukopa bila kulazimika kuweka dhamana ya mikopo hiyo.

Wito huo ulitolewa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka eneo la Fela mkoani Mwanza hadi Isaka mkoani Shinyanga.

Alisema mikopo hiyo ni sehemu ya benki hiyo kushirikiana na serikali katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maendeleo na malengo ya Taifa kiuchumi na kijamii.

"Tumeshirikiana na kampuni za kigeni zinazoratibu miradi mikubwa kama ujenzi wa barabara, pamoja na miundombinu ya maji...mpaka sasa tumetoa dhamana ya zaidi ya Sh. bilioni 200 kwenye mradi wa reli ya kisasa (SGR). NMB imefanikisha zabuni kwa makandarasi wazawa zaidi ya 500 katika ngazi ya wilaya na mikoa," alisema Zaipuna.

Alisema NMB imewezesha manunuzi ya nje ya Shirika la Umeme (TANESCO), Mamlaka ya Bandari (TPA) na Bahari Kuu la Dawa (MSD) kwa kutumia Letters of Credit zenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 120.

"Tayari tumetoa dhamana ya Sh. bilioni 48 kwa kampuni za wazawa zinazotekeleza miradi ya umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini, REA," alisema Ofisa Mtendaji mkuu huyo.

Pamoja na huduma za kifedha, benki ya NMB pia inashirikiana na Serikali kupitia Shirika la Reli (TRC) kulipa fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yanapitiwa na miradi ya ujenzi wa reli.

# Mitaala ya masuala ya watoto yapendekezwa vyuo vya habari

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

JUKWAA la Wahariri Tanzania (TEF) limevitaka vyuo vya uandishi wa habari kuweka na kufundisha mitaala inayohusu masuala ya watoto na kupinga ukatili wa kijinsia, ili waitumie vyema elimu kusaidia wimbi kubwa la watoto na vijana linalokumbwa na majanga.

Limesema kwamba haki hiyo inarudisha nyuma maendeleo yao hasa kielimu.

Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, alisema hayo jana mkoani hapa wakati akizungumza na wadau wa vyuo vya uandishi wa habari nchini likiwamo Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), ambapo alisema kwa kutumia vyombo vya habari, jamii inaweza kubadilika na kuelimisha watoto kwa kina madhara mbalimbali yanayoweza kuwakumba, hivyo kuokoa watoto wengi kupoteza mwelekeo wao kimaisha. Alisema lipo kundi kubwa la watoto na vijana ambao hujikuta wakipata mimba za utotoni na wengine kuingizwa kwenye makundi ya madawa ya kulevya, na kwamba vyombo vya habari vikiendelea kutoa elimu ya madhara ya matendo yasiyofaa kwao, itawasaidia wao na jamii nzima kubadilika.

Balile alisema pia wamefungua mipaka ya kutoa elimu hiyo kwa jamii kwa kuanzisha Jukwaa la Wahariri Afrika Mashariki (EAES), ambapo wameanza kwa kushirikiana na Kenya na watashirikiana na nchi zingine kuhakikiasha suala la ukatili wa kijinsia linakomeshwa.

Naye Mtaalamu wa Elimu kutoka NECTA, Dk. Emmanuel Mahenya, alisema wameshaweka miongozo ya kuingiza ajenda za mitaala ya watoto kwenye vyuo nchini, ambazo zitavifanya vyuo kuendelea kutoa elimu hiyo bila kusita kwa wanavyuo.



Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'A', Mkoa wa Kaskazini Unguja, Sadifa Juma, akikagua moja ya chumba cha vyoo vya Shule ya Awali, Msingi na Sekondari ya Kandwi iliyoko Unguja, Zanzibar, baada ya kufanyiwa ukarabati mkubwa na Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation (AMF) kwa hisani ya Benki ya Exim. Ukarabati huo umegharimu Sh. milioni 10. Wanaoshuhudia ni Meneja Mwandamizi wa Exim Zanzibar, Mwinyimkuu Ngalima (kulia) na Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa AMF, Asma Mwinyi (katikati). **MPIGAPICHA WETU**

# Msaada wa kisheria kwa wananchi warahisishwa

**Na Frank Monyo**

SHIRIKA linalofanya kazi ya kukuza upatikanaji wa haki nchini kupitia uwezeshaji wa kisheria (LSF) limezindua mfumo wa kitumizi cha simu za mkononi unaojulikana kama HAKI YANGU App, ambao, unaweza kumsaidia mwananchi kupata msaada wa kisheria popote alipo kupitia simu yake.

HAKI YANGU App ni mfumo wa kwanza nchini uliobuniwa na LSF, ambao umewaunganisha wasaidizi wa kisheria takribani 4,000 nchi nzima, ambapo kupitia mfumo huo wanaweza kukutanishwa na mwananchi mwenye uhitaji wa huduma za msaada wa kisheria ama wasaidizi wa kisheria kwa kutuma ujumbe mfupi wa maneno au kupiga simu, na kuweza kumsaidia.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mfumo huo jijini Dar es Salaam, Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema, LSF imekuwa ni mdau muhimu wa serikali hasa katika sekta ya msaada wa kisheria kwa kuwa imekuwa mstari wa mbele kuwezesha upatikanaji wa haki kwa wananchi kupitia mradi wake wa upatikanaji wa haki.

"LSF imekuwa ikichagiza mabadiliko ya kisera na kimfumo katika sekta ya msaada wa kisheria kwa kushirikiana kwa karibu sana na serikali. Mwaka 2017 tulishirikiana kwa karibu katika kuhakikisha sheria ya msaada wa kisheria inatungwa ili kuwezesha wananchi wetu kupata haki zao kupitia huduma za msaada na wasaidizi wa kisheria."

"Pia leo nimefurahi kuona LSF wamekuja na mfumo ambao utasogeza huduma karibu zaidi kwa wananchi wanaohitaji huduma ya msaada na wasaidizi wa kisheria," alisema Prof. Kabudi.

Aliongeza kuwa serikali inatambua mchango walionao wadau wa maendeleo nchini ikiwamo sekta binafsi pamoja sekta ya mashirika yasiyo ya kiserikali katika kuunga juhudi za serikali kwenye kuboresha huduma mbalimbali za kijamii, ikiwamo huduma ya msaada wa kisheria na upatikanaji wa haki kwa ujumla kwani ni muhimu katika kuchochea maendeleo ya kijamii na uchumi kwa ujumla.

"Naipongeza sana LSF kwa kuendelea kushirikiana na serikali katika suala hili la kutafsiri sheria kwa lugha ya Kiswahili na kwa kuendelea kutekeleza mradi wake mkubwa Tanzania, ambao kwa kiasi kikubwa umeweza kusaidia maelfu ya wananchi walio kwenye mazingira magumu hususani wanawake na watoto kupata haki zao kutokana na kazi nzuri inayofanywa na wasaidizi wa kisheria nchi nzima."

Kwa upande wake, Ofisa Mtendaji Mkuu wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alisema, LSF imebuni mfumo wa HAKI YANGU App ili kuendelea kuhakikisha huduma za msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria nchini Tanzania zinapatikana kiurahisi zaidi kwa kuwa, upatikanaji wa huduma hiyo imekuwa ni changamoto katika jamii licha ya umuhimu wake.

"Kwa uzoefu wa LSF katika kutekeleza mradi wa upatikanaji wa haki nchini tumeona kuwa, wananchi walio wengi bado wanakumbana na changamoto mbalimbali ikiwemo vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto hivyo njia hii itachochea upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa urahisi zaidi mahali popote kupitia simu ya mkononi.

# Mikoa yenye tishio kwa malaria yapungua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imefanikiwa kupungua kwa idadi mikoa yenye hatari kubwa ya maambukizi ya malaria kutoka mikoa 11 mwaka 2017 hadi mikoa saba mwaka 2020.

Aidha, visa vipya vya malaria vimepungua kwa asilimia 35 kutoka wagonjwa 162 kwa kila watu 1000 mwaka 2015 hadi wagonjwa 106 kwa watu 1000 mwaka 2020.

Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Dorothy Gwajima, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji uwepo wa kiwanda cha kuua mazalia ya mbu (TBPL) kimesaidia vipi mapambano dhidi ya malaria nchini.

Akijibu, Dk. Gwajima alisema tangu kiwanda hicho kuanza uzalishaji mnamo mwaka 2016, jumla ya lita 340,520 za viuadudu zimenunuliwa na serikali kwa gharama ya Sh. bilioni 4.5 ambazo ni wastani wa Sh.13,200 kwa lita.

"Lita hizi za viuadudu zilisambazwa katika mikoa 28 na kufikia halmashauri zote 185 nchini. Juhudi hizi ziliungana pamoja na utekelezaji wa afua zingine za udhibiti wa malaria zikiwamo matumizi ya vyandarua, kupulizia viuatilifu-ukoko ndani ya nyumba (IRS) hasa kwenye maeneo yenye kiasi kikubwa cha maambukizi ya malaria na uwapo wa vipimo na dawa zenye ubora kwenye kutibu wagonjwa watakaothibitika kuwa na malaria," alisema.

Hata hivyo, alisema matokeo ya juhudi hizo zimefanikisha kupungua kwa idadi ya mikoa yenye hatari kubwa ya maambukizi ya malaria.

"Naomba kumthibitishia Mhe. Mbunge na Bunge lako tukufu kuwa serikali itaendelea kutumia bidhaa za Kiwanda chetu cha Kibaha (TBPL) kwa ajili ya kuchangia jitihada za serikali kufikia kumaliza malaria nchini ambapo tumedhamiria kuwa ifikapo 2025 kiwango cha malaria kiwe kimepungua hadi kufikia asilimia 3.5 kutoka asilimia 7.5 ya mwaka 2017," alisema.

Aidha, alisema serikali itahakikisha kila halmashauri inawajibika kwenye kuhakikisha kuwa inatenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya utekelezaji wa zoezi hilo kila mwaka wa fedha ambapo Sh. bilioni 2.7 zimetengwa kwa mwaka 2021/22.



Wabunge (kutoka kushoto), Daniel Sillo (Babati Vijijini), Festo Kiswaga (Kalenga), na Miraji Mtaturu (Singida Mashariki), wakimsikiliza Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini, David Kihenzile, walipokutana nje ya ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Miradi sita ya mabadiliko tabianchi yaombewa fedha

BUNGE limeelezwa kuwa hadi sasa miradi sita ya mabadiliko ya tabianchi imeombewa fedha kutoka Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi kupitia taasisi mbalimbali.

Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Hamad Hassan Chande, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Donge (CCM), Soud Mohammed Jumah.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji taasisi ngapi zimeweza kujisajili hadi sasa na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi nchini na miradi mingapi imeshaombewa kupitiwa mfuko huo.

Akijibu, Naibu Waziri Chande alisema ni miradi miwili kati ya hiyo ambayo fedha yake imeidhinishwa.

"Miradi hiyo ni mradi wa maji kwa Kuwezesha Uhimili katika Mkoa wa Simiyu Dola za Marekani 120 millioni na Mradi wa Kuandaa Uwezo wa CRDB Dola za Marekani 560,000," alisema.

Awali, alibainisha kuwa mfuko huo ulianzishwa mwaka 2010 na kuanza kufanya kazi mwaka 2015 na taasisi inayotaka kuomba fedha kutoka katika mfuko huo ni lazima iwe imesajiliwa au kupata ithibati chini ya mfuko huo.

"Ithibati au usajili hutolewa baada ya taasisi husika kutimiza vigezo stahiki, mfuko unaruhusu taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa kusajiliwa ili kuweza kuomba fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Hata hivyo, alisema hadi kufikia mwezi Machi 2021, mfuko huu ulikuwa umesajili jumla ya taasisi 74.

"Hapa nchini, taasisi iliyopata usajili ni moja tu, ambayo ni Benki ya CRDB, tunaipongeza CRDB kwa kuweza kupata ithibati ya mfuko huu, kwa kuwa usajili wa taasisi katika Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi hauna ukomo, serikali inaendelea kuhamasisha taasisi nyingine za hapa nchini kujisajili na mfuko huu ili kuwa na uwezo wa kupata fedha na kutekeleza miradi ya mabadiliko ya tabianchi," alisema.

# Utekelezaji agizo la Samia mikopo halmashauri rasmi

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema imeanza kutekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuhusu utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa kuagiza halmashauri zitoe mikopo yenye tija kwa wajasiriamali ili wajikwamue.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Dk. Festo Dugange, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Zaytun Swai.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema Rais alivyokuwa anazungumza na wanawake aliagiza halmashauri zitoe mikopo mikubwa kwa vikundi ili kuondeza tija kwa mikopo hiyo na kuhoji lini halmashauri zitaanza kutekeleza maagizo hayo.

"Pia kumekuwa na urasimu mkubwa katika kupata mikopo ya halmashauri wanufaika wanatembea umbali mrefu kufuatilia mikopo bila mafanikio," alisema.

Akijibu, Dk. Dugange alisema tayari ofisi hiyo imeanza kutekeleza hilo kutokana na Rais Samia kuweka msisitizo kuhakikisha mamlaka za serikali za mitaa zinatoa mikopo yenye tija kwa vikundi vya wajasiriamali ambao ni wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji serikali haioni umuhimu wa kuweka uwiano sawa wa mikopo ya asilimia 10 inayotokana na mapato ya ndani bila kujali mapato ya halmashauri husika ili kusaidia wanufaika wa mikopo wanaoishi nje ya miji wapate fursa sawa na wanufaika wa mijini.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Dugange alisema mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura ya 290 Kifungu cha 37A na Kanuni zake za mwaka 2019.

"Msingi wa Sheria ya Mikopo ya asilimia 10 ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ni asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri baada ya kuondoa mapato lindwa. Hivyo kiwango cha mikopo kinatokana na uwezo wa makusanyo ya halmashauri husika," alisema.

Alisema halmashauri zimeelekezwa kutoa fursa sawa za mikopo kwa vikundi vyote vilivyokidhi vigezo vilivyopo ndani ya halmashauri husika na kwamba mikopo hiyo ni sehemu tu ya mifuko mbalimbali ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi iliyopo nchini na serikali itaendelea kuiboresha kadri itakavyohitajika.




**Habari zote na Augusta Njoji, DODOMA**

# ama


ALHAMISI JUNI 17, 2021

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Kinamama wakinga sikio, wanena ulivyo ubia bajeti taifa, afya jinsia**



Ukurasa 14

UTAFITI MADINI SHINYANGA...

**Uchimbaji holela madini unavyoharibu mazingira, wenye ulemavu wadai waboreshe**

# Mjue mrembo anayeteswa jasho kumtiririka saa zote, harufu kali

- Kwapa, mikononi, nyayo, harufu ya viatu...
- Alikimbiwa sana, akampata 'wa boga na ua'

**Na Mwandishi Wetu**

ANA wasifu kuanzia baba mzazi na hata kaka za mwanamama Everlyne Juma, wote wana kawaida ya kutokwa jasho jingi siku nzima.

Kwa mbali anaonekana wa kawaida kwa umbo na urembo, ila anapokaribia hali hiyo anayogundua kuwa amelowa jasho karibu mwili mzima, kuanzia usoni, miguu na kwapa zake. Ndio hali ya maisha yake kila siku.

Everlyne Juma, anaishi ana ugonjwa wa kutokwa jasho jingi kupita kiasi mwili, ujulikanao kwa lugha ya kitaalamu 'hyperhydrosis' akisema ni hali aliyozaliwa nayo.

Anasimulia, alipokua familia yake iliona hali yake jambo la kawaida, pia naye akiichukulia katika hali hiyo.

Alipokuwa katika shule ya msingi jijini Nairobi Kenya, ndipo aligundua kalamu yake iliteleza na kitabu chake kililoa jasho lake lililoendelea kutiririka muda wote darasani.

Hapo akakutwa na wakati mgumu wa namna ya kuvaa viatu vya kawaida shuleni, kwani ililoa maji, huku wazazi hawakuwa na uwezo wa kumnunulia viatu zaidi ya kimoja. Ilibidi akubali hali yake, akiingia mbadala wa kuvaa kandambili.

Hali anasimulia kingine cha kero kilichoibuka, pale jasho lilipochanganyika na na mchanga, ilimlazimisha kunawa miguu kila alipowasili shuleni.

Baadaye alijiunga na elimu ya sekondari ya bweni. Hapo ndipo mambo yalianza kubadilika, kwa sababu alilazimika kuvaa viatu vya kawaida vya sare ya shule vya kufunika miguu yake.

Ni ndani ya mwezi mmoja alipojiunga na sekondari, tayari viatu vyake vilianza kutoa harufu mbaya na katika kujisitiri, alibuni mbinu za kuwaficha wenzake wasijue ulivyo uvundo katika viatu vyake.

Hata hivyo, haikuchukua muda tetesi zikaanza kusambaa kuhusu jasho na ukakasi wake. Anaendelea: "Wakati mmoja nakumbuka ni wakati tulikuwa tunajitayarisha na mazoezi katika klabu ya utumbuizaji, pale sisi sote hatukuwa tumevaa viatu.

"Kila zamu yangu ilipowadia niliponyanyua miguu nyayo zangu zilichora unyevunyevu, baadhi ya wenzangu pale walinong'onezana huyu ana nini anamwaga maji ovyo ovyo?

"Maneno hayo yaliniumiza sana, yalinifanya nichukue uamuzi wa kuondoka katika klabu hiyo ya burudani, ile siku ilikuwa ya kwanza na ya mwisho niliachia pale ..."



Ndiye mrembo, Everlyne Juma. **PICHA: MTANDAO.**

Anasema, kwani hata kuwasalimia watu kwa mikono ilikuwa shida, kwani ililoa jasho jingi. Hivyo, alichukua uamuzi wa kutowasalimu watu kwa mikono.

"Nilielewa fika jinsi mila na desturi za Waafrika zilivyo kuhusu umuhimu wa kumsalimia mtu kwa kumpa mkono, ilikuwa changamoto kubwa sana kwangu. Wengi waliniona kama binti asiye na nidhamu, wengi walinitazama tu kwa kunikejeli," anasimulia Everlyne.

Anakumbuka tafakari yake: "Kila kukicha huwa ninapanga jinsi nitakabiliana na hali hiyo pindi jasho likianza kutoka... hakuna saa maalum ambayo ninaweza kusema jasho litatoka. Jasho linaweza kutoka asubuhi usiku au mchana na wakati mwingine hata mchana kutwa."

Wasiwasi na woga aliyoishi nayo shuleni, ndio alihama nayo alipojiunga na taasisi ya mafunzo ya mawasiliano. Hapo nako alihisi mtihani katika maisha yajayo, atakapobahatika kuajiriwa.

Upande mmoja anakumbuka hulka ya kuajiriwa mwanahabari, ila akarejea magumu kazini, kutokana na jasho lake. Alikata tamaa, akaachana na ndoto hiyo.

Anasema, kuna wakati aliamua kuajiriwa kwa nafasi mhudumu wa mapokezi katika ofisi mojawapo. Wapo wanaume aliokutana, walihitaji kuwa na uhusiano naye, ila walipobaini harufu ya jasho mwilini, iliwakatisha tamaa na wapo waliomkimbia.

**AFANIKISHA NDOA**

Kutoka usemi 'Mungu si Athuman,' hatimaye alipata mume aliyempenda, mtu waliyefahamiana mtaani na hatimaye wakafunga ndoa.

"Baba wa watoto wangu wawili na ambaye ni mume wangu, hakuonekana kushtushwa na jasho langu. Yeye alisimama nami wakati wote wa uchumba wetu na hadi sasa miaka mingi baadaye ndoa yetu ingali imara," anasema Everlyne.

Everlyne anasema kuwa amepata ujasiri wa kuzungumzia hali yake bila ya uoga, hali aliyoishi nayo miaka 32, pale amejikubali.

Hofu aliyo nayo ni kwamba bintiye tayari ameshaanza kuonyesha dalili za kuwa na tatizo hilo. Anafafanua: "Ninapomtazama binti wangu ninaona haja ya kujitokeza kwa umma kuzungumzia ugonjwa huu wa kutoa jasho jingi kila wakati, kwani nimepita changamoto nyingi hadi nilipo hivi sasa.

"Ni katika harakati hizi mimi na baadhi ya Wakenya wanaoishi na hali hii tuliunda muungano wetu ambao ungetupa fursa ya kusaidiana na pia kupeana nguvu."

**ULIVYO UGONJWA HUO**

Jasho la kupindukia linalohusiana na maradhi 'hyperhidrosis' kawaida hutokea kwenye mikono, miguu, kwapa na sehemu zilizonepa mwilini, kwa sababu ya viwango vyake vya tezi za jasho.

'Hyperhidrosis' inakuwapo tangu kuzaliwa au inaweza kujitokeza baadaye maishani. Ila, mara nyingi

Endelea Uk. 14

AFYA

# Kinamama wakinga sikio, wanena ulivyo ubia bajeti taifa, afya jinsia

## •Wapiga makofi, huku wakidai 'bado hili'

**Na Yasmine Protace**

BAJETI Kuu ya Serikali ya mwaka huu iliyosomwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba,

imewasilishwa wiki iliyopita ikiwa na sura ya mabadiliko yenye maboresho katika baadhi ya sekta.

Ndani ya bajeti hiyo, wapo baadhi ya wadau kutoka asasi za kiraia kwa kushirikiana na TGNP Mtandao na vikundi vya kijamii kutoka mikoa mbalimbali, sasa wametoa maoni kupitishwa bajeti hiyo ya serikali.

Kimsingi, Bajeti Kuu ya Serikali ni kielelezo cha namna serikali inajipanga kupendekeza mwelekeo wa

katika sekta mbalimbali zitagharamiwa, ili kuleta mabadiliko kitaifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, anasema kuwa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa kushirikiana na wadau, asasi za kiraia na vikundi vya kijamii kutoka mikoa mbalimbali, wanahusika.

Katika majumuisho yake akiwa na jicho la kipekee, anafafanua: "Mnamo tarehe 10 Juni mwaka huu, kupitia mjadala wa Bajeti ya Taifa, tulifuatilia kwa pamoja

na kuchambua bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 iliyokuwa ikiwasilishwa bungeni na Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Lameck Nchemba."

Anarejea majukumu ya mashirika yanayotetea

haki za wanawake, yamekuwa wakipigania kwa muda mrefu usawa wa kijinsia, hivyo wanaipongeza

serikali kwa kuchukua hatua kutekeleza kilio chao na

kusimamia utekelezaji wa sera na mipango ya maendeleo kwa manufaa ya taifa na raia wake.

**HAKI JINSIA**

Lilian anaongeza kuwa maeneo yaliyoguswa nayo yanajumuisha sekta ya afya na penye maboresho ya ujenzi wa zahanati 1,198 , jengo la 'Mama na Mtoto' katika katika Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala Dar es Salaam, sasa inafika asilimia 51 kukamilika.

Pia katika mkoa wa Simiyu, anataja hatua hizo zimechangia kupunguza vifo vya kinamama na watoto na kuna magumu katika upatikanaji huduma za uzazi salama bila ya gharama, kwa kuwapo tozo hususani kwa wahitaji wa upasuaji.

Mkuu huyo wa TGNP Mtandao,



Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, alipozungumza baada ya kuwasilishwa kwa makadirio ya Bajeti ya Kuu ya Serikali, mwaka huu. **PICHA: YASMINE PROTACE**

anasisitiza kwamba wanawake ndio wanaoleta nguvu kazi za kitaifa na hawapaswi kulipa gharama, kwani ili taifa taifa lisonge mbele kuna haja ya kinamama, kuthaminiwa kupitia kazi yao nzito.

Pia upande wa pili analalamika upungufu wa vituo vya afya na zahanati kwenye baadhi ya maeneo vijijini na mijini, ni jambo linalosababisha changamoto kubwa kwa wajawazito, hasa waliofikia hatua ya kujifungua.

Katika angalizo lake, mkuu huyo wa taasisi hiyo ya kijinsia, analalamika bajeti pia haijaainisha kiwango

ilichojipanga kupunguza upungufu wa watumishi wa afya, kwa baadhi ya vituo vya afya hasa vijijini.

Anatoa mfano kuwapo baadhi ya vituo havina hata huduma za maji na umeme.

**MAJI/ MAHITAJI JINSIA**

Katika suala la upatikanaji huduma za maji, serikali imefanikiwa kumtua ndoo mama vijijini na mijini kwa asilimia 72.3 na 85 kufikia kukamilika miradi 1845 ya maji, vijijini na mijini.

Anasema, bado tatizo la huduma ya maji na ugumu wake kwenye maeneo mengi hususani vijijni wanakoshi wanaishi, pia katika mazingira yenye huduma za umma kama vile vituo vya afya na taasisi za elimu.

Lilian anapendekeza serikali kuelekeza Sekta ya Maji kutanua na kuuwezesha mtandao wa huduma za maji safi na salama, kwa kuweka mikakati ya upatikanaji fedha zitakazowezesha suala hilo.

Pia, anaitaka Sekta ya Maji iondoe tozo za maji kwa taasisi za umma kama shule na vituo vya afya na wizara itoa maelekezo kwa idara za maji za mikoa kuwezesha upatikanaji maji kwa wajane na wazee, kwa tozo zenye viwango vya chini, au pasiwapo tozo, hali hiyo ifike hadi pasipo gharama.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akionyesha mkoba wa Bajeti Kuu ya Serikali, bungeni wiki iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

Lilian anasema katika kumkomboa msichana shuleni, bajeti imeendelea kuwa kimya katika upatikanaji wa taulo za kike na miundombinu ya hedhi salama kwa wanafunzi wa kike, walio kwenye elimu ya msingi na sekondari.

Anasema bajeti haijataja mafungu au kutoa maelekezo yoyote kwa halmashauri za wilaya, au mamlaka za elimu kuyazingatia mahitaji hayo.

"Katika mafungu ya fedha wanayopata. Kuna umuhimu wa serikali kutoa maelekezo ya kuwezesha upatikanaji

wa bajeti hii, ili kuwasaidia wanawake na watoto wa kike kuondokana na fedheha na changamoto za kiafya

wanazokutana nazo, wakiwa katika hedhi kwa kukosa vifaa safi na salama vinavyojisitiri wakiwa katika hedhi," anasema.

Anaendelea kutoa wito kwa usawa wa jinsia, kwa kuondolewa tozo katika miundombinu ya hedhi salama kwa wanafunzi wa kike, walio na mfumo wa elimu ya msingi na sekondari.

Lilian anasema bajeti haijataja mafungu au kutoa maelekezo kwa halmashauri za wilaya, pia mamlaka za elimu kuyazingatia mahitaji hayo katika mafungu ya fedha wanayopata.

Angalizo lake lingine ni katika umuhimu wa serikali kutoa maelekezo ya kuwezesha upatikanaji wa

bajeti kuwasaidia wanawake na wasichana kuondokana na fedhea za kiafya wanazokutana nazo, wanapokuwa katika hedhi, hasa kukosa vifaa safi na salama vya kujistiri.

Mama huyo anasema, wanaendelea kutoa wito kwa iliyoko madarakani, wanayoitaja inatambua usawa wa kijinsia wakiitaka iondoe tozo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye pedi ilirudishwa mwaka 2019.

Lilian anaeleza kwamba, kuna haja ya serikali kutenga bajeti inayolenga kuhamasisha utoaji kwa wajane, wazee na wanawake na kaya maskini nchini.

Anasema,kwa sasa wanaikumbusha serikali kuhimiza makubaliano ya Abuja, Nigeria iliyoridhia haja ya kila serikali kutenga asilimia 15 ya bajeti kuu, kwa jili ya huduma ya afya.

"Tunatoa wito kwa serikali na wadau wengine kuongeza

uwekezaji katika kutoa elimu ya umuhimu na namna ya kuzuia magonjwa, ili kupunguza gharama za

matibabu ya magonjwa yanayozuilika," anasema.

AFYA

# Kukata tamaa kunavyodhuru wengi wakati wa kutibu ugonjwa saratani

## •Wadau wabuni faraja, sherehe maalum

**Na Mwandishi Wetu**

NIKIWA mwenye umri wa miaka 29 nilipimwa hospitalini nikabainika kuwa ninaugua saratani ya mlango wa kizazi.

Ni taarifa zilizonishtua kuliko matukio yote yaliyowahi kunipata maishani mwangu. Hata ndugu na jamaa walipopokea kwa tafsiri kwamba siku zangu za kufa zimekaribia.

Kwa sababu hiyo, maelekezo na ushauri ulikuwa mwingi, miongoni wakiniasa nisithubutu kupata matibabu hospitalini, kwa madai hiyo itakuwa ni tiketi ya kuniua mapema.

Baadhi walinishauri nikapate matibabu kwa waganga wa kienyeji, wengine wakataka nikaombewe kanisani wengine kwa sheikh, wengine niendelee na ushauri hospitalini na baadhi kushauri nifanye hayo yote kwa pamoja.

Ni maelezo ya Amina Moleli, mkazi wa Arusha akisimulia yaliyomkuta mara baada ya kuchunguzwa na kudhihirishiwa na wataalamu wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), kuwa ana saratani ya mlango wa kizazi mwaka 2013.

Anaelezea ni mazingira ambayo yalimfanya achanganyikiwe na kuona ndio mwisho wa maisha yake na hata kuona kuwa ndoto mbalimbali za kimaisha alizokuwa amejiwekea hazina tena maana.

Mama huyo akiwa kwenye wimbi hilo la mawazo, akakumbuka daktari aliyemthibitishia kuwa ana saratani alimshauri awe mtulivu, azingatie tiba na awe na imani kwa uwezo wa Mungu, atapona na kurejea tena kwenye maisha yake ya kawaida.

Hata hivyo, alikata shauri kwamba afuate ushauri wa daktari wake licha ya vitisho wagonjwa wengi wa saratani waliofuata taratibu za kihospitali walipoteza maisha.

"Nakumbuka niligundulika kuwa na saratani ya mlango wa kizazi mwaka 2013 na nikaanza matibabu (ORCI) Agosti 11, 2014 na nashukuru sasa nimepona kabisa," Amina anatamka, akiwa na ufafanuzi zaidi kuwa:

"Kwa kweli matibabu ya saratani ni makali sana, yanaandamana na maumivu na changamoto nyingi sana kiasi kwamba, kama hauko imara, unaweza kukata tamaa. Nashukuru madaktari na wauguzi walinipa moyo."

Anasimulia katika kipindi cha matibabu, alipata fursa ya kubadilishana mawazo na wagonjwa wa muda mrefu zaidi ya miaka mitano, wakamshauri asishawishike kupata tiba za asili kwa sababu miongoni mwao waliofanya hivyo tayari wameshapoteza maisha.

"Wakati nikipata tiba nilimtumainia Mungu na kumuomba anisaidie tiba nilizokuwa napata zinisaidie. Nashukuru hivi sasa nimepona kabisa," anasimulia Amina.

"Kwa sasa naishi vizuri na mwenza wangu wa ndoa na nafanya kazi zangu vizuri na sina wasiwasi na ndoto zangu za kijasiriamali zinaenda vizuri," anaeleza.



Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Shujaa Cancer Foundation, Gloria Kida, alipozungumza kwenye sherehe za Siku ya Mashujaa wa Saratani, jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Meneja Bidhaa wa Benki ya KCB na wa kwanza kulia, Mkurugenzi wa Tiba wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dk. Mark Mseti na Sheikh Yakubu Bakari. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

### BINGWA OCEAN ROAD

Namna ilivyo kuhusu tiba za saratani, Mkurugenzi wa Tiba ORCI, Dk. Mark Mseti, anasema huwa wanawahamasisha wagonjwa wao kuwa na moyo wa uvumilivu na kufuata kile wanachowaelekeza iwapo kweli wameazimia kupona.

Anasema wanawaweka wazi wagonjwa kuwa wakati mwingine matibabu huchukua muda mrefu na kuna wakati wanafanya mabadiliko ya aina ya tiba au yanachanganywa kwa pamoja.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Mseti anasema maumivu na tiba za muda mrefu, huweza kumfanya mgonjwa anakata tamaa.

"Mgonjwa anayetibiwa saratani akiruhusu tu kukata tamaa inakuwa rahisi kupoteza maisha. Ukishinda kwenye hii vita wewe ni shujaa," Dk. Mseti anatoa agalizo la kisaikolojia.

Anasema matibabu ya saratani ni vita vya muda mrefu, inayobeba mapigano mengi na walioshinda kwenye vita hiyo, wanapaswa kushangilia na kujiita mashujaa.

Dk. Mseti anasema, saratani ni ugonjwa unaojumuisha magonjwa mengi ambayo yanafanana kwa kuwa na chembe hai za mwili zinazozaliana kwa haraka bila ya udhibiti na zinasafiri mwili na kwenda kuzaliana katika eneo jingine.

Anafafanua kuwa chembe hai hizo za kawaida za mwili, haziwezi kuhamishiwa kwenye kiungo kingine tofauti na cha awali na kuendelea kuzaliana kama zilivyo za saratani.

"Mfano ukichukua seli za ulimi ukiziweka kwenye mkono haziwezi kuendelea kuishi. Lakini, seli ya saratani popote utakapoziweka mwilini zitaendelea kuishi na kuzaliana," anafafanua upekee wa maradhi hayo.

Kuhusu visababishi vya saratani, Dk. Mseti anasema vipo vya aina nyingi na miongoni ni kemikali, mionzi, urithi wa vinasaba na mtindo wa maisha kwa maana uwiano wa vyakula anavyokula na suala zima mwili unavyojishughulisha.

### INAVYOKUJA NA KUKABILIWA

Kula kwa wingi vyakula vyenye sukari, wanga, mafuta, protini na kutofanya mazoezi, anaelezea ni moja ya chanzo cha kunenepa na kuwa na uzito kupita kiasi hivyo kuwa rahisi kupata magonjwa yasiyoambukiza mfano saratani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Shujaa Cancer Foundation (SCF), Gloria Kida, anasema kuanzia mwaka huu kila Jumapili ya kwanza ya Juni Tanzania itakuwa inaadhimisha Siku ya Mashujaa wa Saratani.

Dhumuni la kuadhimisha siku ya mashujaa, ambayo imekuwa ikiadhimishwa na mataifa mengi duniani kwa miaka mingi, ni kuwatambua watu waliopo kwenye tiba na hata waliopona.

"SCF inamtambua shujaa wa saratani kuwa ni yule ambaye amepata matibabu na amepona au aliyemaliza matibabu ya awali na anaendelea na hatua nyingine," anasema Gloria.

Hii ni kwa sababu wanajua kwamba tiba wanazopitia siyo nyepesi na zinaandamana na kupata maumivu makali na shida mbalimbali.

Anasema hata baada ya tiba kuna athari ambazo huwa zinajitokeza na kuzidi kumweka mgonjwa katika wakati mgumu.

"Ni siku ya kufurahia maisha wakati na baada ya tiba kama ilivyo kwa watu wanaofanya sherehe ya kukaribisha ndugu jamaa na marafiki katika kuadhimisha siku ya kuzaliwa au kukamilisha jambo muhimu katika maisha," anasema.

Anailezea SCF kuwa ni asasi ambayo lengo lake kuu ni kuwahudumia mashujaa wa saratani ya via vya uzazi, yaani ya matiti, tezi dume na mlango wa kizazi mara wanapomaliza tiba ya awali.

SCF analenga katika kuainisha changamoto wanazopitia mashujaa wa saratani ya via vya uzazi na kuratibu njia mbalimbali za kuwasaidia namna ya kukabiliana na vikwazo hivyo.

Anasema uzoefu wa SCF unaonyesha kwamba wagonjwa wa saratani wanahitaji kupewa ushauri nasaha wakati wote wa tiba na hata baada ya kupona kabisa.



Mkurugenzi wa Tiba Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dk. Mark Mseti, alipohutubia katika sherehe za Mashujaa wa Saratani jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji Mtendaji wa Asasi isiyo ya kiserikali ya Shujaa Cancer Foundation (SCF), Gloria Kida na kulia, Sheikh Yakubu Bakari.

MAZINGIRA

## UTAFITI MADINI SHINYANGA...

# Uchimbaji holela wa madini unavyoharibu mazingira, wenye ulemavu wadai waboreshe

- Ni kupitia ajira maalum kisheria
- Ofisa Madini: Upandaji miti tatizo

**Na Marco Maduhu, KAHAMA**

MIGODI midogo ya madini ya dhahabu, kwa sehemu kubwa inachangia kuharibu mazingira, kutokana na kutawaliwa na uchimbaji wa kukisia uwapo wa madini, inayoishia kuachwa mashimo.

Mgodi wa Mwanzimba uliopo Msalala wilayani Kahama, tayari mazingira yake yameshaathirika kutokana na awali kabla ya kupatikana leseni, kulikuwapo na uchimbaji holela wa madini.

**MENEJA MGODI**

Meneja wa Mgodi huo wa Madini, Mwanzimba Ndembuke, anasema mashimo yaliyopo mgodini humo yametokana na awali kila aliyekuwapo alijaribu bahati yake ya kupata madini na hatimaye waliishia kuharibu mazingira.

Anasema, walianza kuchimba mgodini humo mwaka 2007 na baada ya kupata leseni ya uchimbaji, sasa wanafuata sheria na kanuni, inayopafanya pasiwapo mashimo yanayobaki kama ilivyokuwa awali.

"Mgodi huu wa madini, awali kulikuwa na uchimbaji wa uvamizi na katika uchimbaji huo, lazima kutokee tu tatizo la uharibifu wa mazingira," anaeleza Meneja Ndembuke.

Anaendelea na ufafanuzi: "Kila mtu anajaribu bahati yake ya kupata madini na ndio tatizo hutokea la kuacha mashimo ovyo na ukataji miti holela."

"Tunaishukuru serikali kututambua sisi wachimbaji wadogo na kuanza kutupatia leseni za uchimbaji madini, hali ambayo imeanza kusaidia kwa kiasi kikubwa kuzuia tatizo hili la uharibifu wa mazingira, sababu ya kuacha kuchimba madini holela," anaongeza.

**OFISA UTAFITI**

Evans Rubara, ni Ofisa Programu na Utafiti kutoka Taasisi ya Kuendeleza Uchimbaji Mdogo wa Madini Tanzania, anasema ili kuzuia uharibifu wa mazingira kwenye machimbo madogo, kuna haja Wizara ya Madini itoe leseni kwenye maeneo yaliyokwishatafitiwa uwapo wa madini yake.

"Sisi kama Taasisi ya Kuendeleza Uchimbaji Mdogo wa Madini tunaiomba Wizara ya Madini, kabla ya kutoa leseni kwa wachimbaji wadogo wa madini, wahakikishe kama kweli sehemu hiyo kuna madini kwa kutumia vipimo vya kitaalamu, ili kusitokee uharibifu wa mazingira," anasisitiza.

Anafafanua kwamba, ni kawaida wachimbaji wadogo wamekuwa na tabia ya kuhama na kwenda kwingine, hasa wanapogundua mahali husika madini hayapatikani na hali inatokea wakati wameshaharibu mazingira kuwa na mashimo na eneo la jangwa.

**OFISA MADINI**

Marwa Geteny kutoka Ofisi ya Madini Mkazi wilayani Kahama, ambaye ndiye mtoaji leseni kwa wachimbaji, anafafanua kuwa sheria za madini zinazuia uharibifu wa mazingira, lakini kwa wachimbaji bado tatizo lipo.

Anasema kwa Wizara ya Madini inahamasisha wachimbaji wadogo wajiunge kwenye vikundi, ili wapewe lesseni ya uchimbaji madini yenye masharti ya kutunza mazingira.

"Utoaji leseni kwa wachimbaji wadogo wa madini utasaidia kwa kiasi kikubwa kuzuia tatizo la uharibifu wa mazingira, kwa sababu kabla ya kupewa leseni ni lazima uje na mpango mkakati wa namna ya kutunza mazingira," anafafanua Geteny.

Pia anafafanua kwamba kwa sasa wanazuia wachimbaji wadogo kuvamia maeneo kuokoa mazingira, bali wachimbe kwenye maeneo yaliyofanyiwa utafiti. Anasema, hadi sasa wameshatoa jumla ya leseni 400 kwa wachimbaji wadogo.



Wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu katika mgodi mdogo wa Mwanzimba, uliopo Msalala wilayani Kahama, wakitumia njia za asili na zana duni katika kazi zao. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

**DC KAHAMA**

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, anawaasa wachimbaji wadogo wilayani kwake kufuata sheria za uchimbaji madini na kwa sasa serikali inawatambua rasmi wachimbaji wadogo wa madini.

Pia anasema serikali imeshawarasimisha, anaendelea: "Naomba Wizara ya Madini na taasisi ya kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini. Toeni elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu namna ya kujua sheria ya madini, utunzaji mazingira, hasa kwa kupanda miti kwenye maeneo yenye mashimo."

**WENYE ULEMAVU**

Mwenyekiti wa Shirikisho la Chama cha Watu wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) wilayani Kahama, Michael Mkanjiwa, anawataka wamiliki migodi wilayani humo kuwaajiri ili nao wafanye kazi ya kutunza mazingira.

Anasema, wenye ulemavu wametengwa sana katika migodini akijiteta bado wana nafasi ya kuajiriwa kwa kazi nyepesi, ikiwamo utunzaji mazingira.

"Sheria ya Ajira ya Watu wenye Ulemavu ya Mwaka 1982, inasema asilimia tatu ya wafanyakazi kwenye eneo lolote lile wanapaswa kuwapo na walemavu. Hivyo, tunaomba kwenye migodi ifuatwe sheria hii, ikiwa tunaweza kufanya kazi nyepesi," anasema Mkanjiwa.

Hosea Mbusule, ni Katibu katika mgodi wa madini ya Dhahabu Mwanzimba, anasema kwa sasa wameshaajiri wenye ulemavu wawili, waliojikita kutunza mazingira.

Anasema shughuli yao kubwa ni usafi wa mazingira, huku wakiangalia namna ya kuajiri wengine wenye ulemavu, pia kupanga mkakati wa upandaji miti kwenye mashimo, ambayo awali yalisababishwa na uchimbaji holela kabla ya kupewa lesseni.

**MTUNZA MAZINGIRA**

Kaimu Ofisa Misitu na Mazingira mkoa Shinyanga, Perfect Mbwambo, anasema hali ya utunzaji mazingira kwenye migodi ya madini na mkoa Shinyanga kwa jumla ni upandaji miti.

Anashauri migodi midogo ya madini iige mfano wa mikubwa, ukiwamo wa almasi Mwadui Williamson Diamond, wenye programu ya kuotesha miti na kutunza mazingira.

Anasema katika mkakati wa kitaifa wa utunzaji mazingira, kila halmashauri nchini inatakiwa kupanda miti na kila halmashauri inapaswa kupanda miti kwa milioni 1.5 kila mwaka, lakini Shinyanga utekelezaji uko chini.

Takwimu za upandaji miti kwa halmashauri sita za za mkoa huo kwa 2019 hadi 2020; Manispaa ya Kahama ilitajwa kupanda miti milioni 1.5 lakini wamepanda 14,000.

Pia, anataja halmashauri nyingine kuwa Kishapu imepanda 160,180; Msalala 91,250; Ushetu 565,979; Shinyanga Manispaa 283,115, na Wilaya Shinyanga, miti 79,000.

## MJUE MREMBO ANAYETESWA JASHO KUMTIRIRIKA SAA ZOTE, HARUFU KALI

**Inatoka Uk. 11**

hali ya kutokwa na jasho kupita kiasi huanza katika umri wa ujana.

Kitaalamu inatajwa haina sababu mahsusi, japo inahusishwa na urithi kutoka wa familia au ukoo.

Dalili zake zinatajwa jasho jingi kutiririka mikononi, kwenye nyayo miguuni, hali inayotokea mara nyingi mwilini, hata kufika hatua ya kulowesha mavazi kupita kiasi.

Kuna watu walioainisha ugonjwa wa 'hyperhidrosis' na imeunganishwa na hali ya akili na joto la mgonjwa, kwamba hali hiyo ilikuwa ya kisaikolojia na iliathiri tu watu wenye msongo, wasiwasi, au woga.

Lakini, utafiti wa hivi karibuni umeonyesha kuwa watu walio na 'hyperhidrosis' hawana tena hisia za wasiwasi, woga, au mfadhaiko kuliko watu wengine wanaopatikana na vichocheo hivyo.

Pia, kunatajwa kuwapo vinasaba mwilini vinavyohusika, hata kuifanya ionekane inaweza kurithiwa. Wagonjwa wanaougua 'hyperhidrosis' wana ndugu au wazazi waliowahi kuwa na hali hiyo.

**NAMNA KUIKABILI**

Wataaluma wanarejea tena hatua kwamba, namna ya kuleta mabadiliko dhidi ya madhara hayo, inajumuisha katika shughuli za kila siku na mtindo wa maisha, kama ifuatavyo:

Eneo mojawapo, ni kutumia vitambaa maalum au hata pedi kuvaliwa kwapani, inafanya kazi ya kunyonya jasho kulinda nguo kulowa.

*Mavazi; mavazi yenye nyuzi na nailoni, yana uwezo wa kudhoofisha dalili za jashi jingi kutoka mwilini. Katika viatu, kuna aina ya asili kama viatu vya ngozi, vinapendekezwa kukabili magumu hayo.

*Pia, soksi si nene na laini zilizotengenezwa na nyuzi za asili kusaidia kufyonza unyevu.

Madaktari wake, hasa kwa mabingwa wa tiba ngozi, washauri iendane kulingana na uhalisia wa ugonjwa.

• *Kwa mujibu wa BBC.*





## Sera ya wazee kupitiwa upya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema iko kwenye mapitio ya Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003, ambayo itaweka msisitizo katika kuimarisha upatikanaji wa haki ya ulinzi na usalama kwa wazee.

Pia imeazimia kuendeleza utekelezaji wa mkakati wa kutokomeza ukatili na mauaji ya wazee nchini.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, aliyabainisha hayo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukatili dhidi ya Wazee.

Alisema hatua hiyo inalenga kutimiza azma ya kuendelea kuwalinda wazee pamoja na kuimarisha huduma nyingine.

Pia alisema kuwa sera inayofanyiwa mapitio inalenga kuimarisha mifumo ya ulinzi shirikishi katika jamii ya kuwalinda wazee kutokana na hatari ya kufanyiwa vitendo vya ukatili, pamoja na mifumo ya upelelezi na uendeshaji wa mashauri ya vitendo vya ukatili na unyanyasaji dhidi ya wazee.

"Kutokana na ukweli kwamba hali duni ya kipato ni miongoni mwa sababu zinazochangia vitendo vya ukatili kwa wazee, serikali inalenga kuhakikisha wazee wanawezeshwa katika kubuni na kuendesha shughuli za ujasiriamali kupitia vikundi vidogo vidogo katika jamii ili kuwawezesha kuinua kipato na kumudu mahitaji yao ya msingi," alisema.

Pia alisema wazee watawezeshwa kushiriki katika shughuli za michezo na burudani ili kuimarisha afya zao na kuwajenga kisaikolojia.

Alisema kutokana na jitihada kubwa zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau, vitendo vya ukatili na mauaji ya wazee nchini vimedhibitiwa kwa kiasi kikubwa.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Jeshi la Polisi, mauaji ya wazee yamepungua kwa kiwango kikubwa kutoka 577 mwaka 2014 hadi wazee 34 Desemba 2020.

Kadhalika, Naibu Waziri alisema kupitia mpango wa serikali wa kuboresha huduma za afya, imeendelea kuhakikisha kuwa kila kituo cha afya cha na hospitali zinakuwa na madirisha maalum kwa ajili ya matibabu kwa wazee ambapo hadi sasa yapo 2,335.

Meneja Programu, Haki na Ushirikiano wa wadau kutoka Shirika la Helpage International Tanzania, Joseph Mbasha, alisema shirika hilo linaamini kuwa kwa kukuza ustawi haki na ujumuishi wazee wataweza kuishi maisha yenye afya, hadhi na salama.

Alisema katika kutekeleza azma hiyo shirika hilo linatekeleza afua tano, ambazo ni kuboresha upatikanaji wa huduma za afya zilizo rafiki na bora kwa wazee.

Alibainisha afua nyingine ni kupinga vitendo vya ukatili na manyanyaso dhidi ya wazee, kutoa huduma jumuishi wakati wa majanga, kuhakikisha usalama wa kipato, pamoja na kuchagiza harakati za mabadiliko.

# TANAPA yaibua mkakati kabambe kukuza utalii

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA), limeandaa mpango mkakati wa miaka mitano unaolenga kutekelezwa kwenye maeneo saba ikiwamo kubuni na kukuza wigo wa bidhaa na mazao ya utalii ili kuongeza idadi ya watalii nchini.

Kamishna Uhifadhi Msaidizi Mwandamizi wa Mawasiliano wa TANAPA, Paschal Shelutete, alibainisha hayo jana kwenye semina iliyoandaliwa na shirika hilo kwa waandishi wa habari Mkoa wa Dodoma.

Alisema shirika linatekeleza shughuli za uhifadhi na utalii kulingana na Mpango Mkakati wa miaka mitano (2018/19 - 2022/23) ambao umefanyiwa marejeo na kuandaa mkakati mwingine wa miaka mitano kuanzia mwaka 2021/22-2025/26.

Shelutete alisema mkakati huo unalenga kutekeleza maagizo ya serikali katika sekta ya utalii nchini.

Alitaja eneo lingine litakalopewa kipaumbele kwenye mkakati huo ni kuimarisha miundombinu ya utalii husussani barabara, viwanja vya ndege, malango, magati, malazi, mawasiliano, maji na umeme.

"Pia kubuni na kuboresha utangazaji wa vivutio vya utalii kupitia televisheni ikiwamo Tanzania Safari Channel ya TBC (Shirika la Utangazaji Tanzania), vipindi vya redio na mitandao ya kijamii," alisema.

Kamishna huyo alisema shirika linatoa pia fursa kwa sekta binafsi katika kuendeleza na kukuza utalii katika hifadhi za taifa, kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi na umma ili kuwekeza katika maeneo ya hifadhi.

"Kuhamasisha jamii ili ijue umuhimu wa utalii na watalii wa ndani watembelee hifadhi za taifa na eneo la saba ni kuimarisha mikakati ya kudhibiti ujangili wa wanyamapori," alisema.

Alisema katika miaka mitano hiyo ijayo shirika limejipanga kuongeza uwezo wa malazi kwenye hifadhi kutoka vitanda 3,429 hadi 5,000.

Akitaja mafanikio mbalimbali yaliyopatikana, Shelutete alisema ni uwekezaji wa puto katika hifadhi za Serengeti, Tarangire na Ruaha, utalii wa 'canopy walkway' katika Hifadhi ya Ziwa Manyara na Kitulo.

"Upembuzi unaoendelea wa kuwekeza katika utalii wa "cable cars" kutoka lango la Machame hadi uwanda wa Shira katika Hifadhi ya Kilimanjaro, pia uwekezaji kwenye miradi ya kimkakati ya kukuza utalii unaoendelea katika hifadhi za Rubondo, Burigi-Chato na Serengeti," alisema.

Awali, akifungua semina hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi Dodoma, Ahmed Mbugi , aliwashauri waandishi wa habari kutumia kalamu zao kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini ili kuhamasisha wananchi kufanya utalii wa ndani.

Aidha, Mbugi alisema baadhi ya wananchi wanaamini kuwa kutembelea vivutio vya utalii ni lazima waende hifadhi za taifa lakini katika Mkoa wa Dodoma na maeneo vipo vivutio ambavyo wananchi wanapaswa kutembelea na kujifunza historia mbalimbali ikiwamo kambi za wapigania uhuru.

Naye Ofisa Uhifadhi Mkuu wa shirika hilo, July Lyimo, alisema utalii husaidia kukuza uchumi na pato la taifa, kutambulisha nchi na kuongeza ajira huku akiwahimiza waandishi kuandika habari za kuhamasisha Watanzania kutembelea hifadhi na kujifunza mambo mbalimbali.



Baadhi ya machifu wa makabila mbalimbali nchini wakifuatilia shughuli za Bunge, walipolitembelea jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kujifunza. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Ataka tathmini nyongeza mkandarasi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Prof. Riziki Shemdoe, ameagiza kufanyika tathmini ya kina ya muda wa nyongeza uliombwa na mkandarasi barabara za Mji wa Serikali Mtumba kwa kiwango cha lami.

Mradi huo kwa sasa ujenzi wake umefika asilimia 70 na unatakiwa kukamilika mwezi ujao lakini mkandarasi huyo, China Heinan International Cooperation Co. Ltd (CHICO), ameomba nyongeza ya miezi 10 ili kukamilisha asilimia 30 iliyobaki.

Akizungumza jana baada ya kukagua ujenzi huo, Prof. Shemdoe alisema mradi huo ulitakiwa kukamilika ndani ya miezi 18 na kwa mujibu wa mkataba mwisho ni Julai 31, mwaka huu.

"Kazi imefanyika tumeiona na kiwango kilichofikia ni asilimia 70. Mradi gharama yake ni Sh. bilioni 89.1 na barabara zinazojengwa jumla ni kilometa 51.2 kazi iliyofanyika ni kubwa. Tunajua hadi Julai 31, hii kazi ya asilimia 30 iliyobaki itakuwa bado haijakamilika. Mkandarasi kuomba nyongeza ya muda wa miezi 10, nimemwagiza mshauri wa mradi huu kwamba pamoja na maombi hayo mimi sitakubaliana nayo ni miezi mingi.

"Kama mradi huu umetumia miezi 16 kujenga kwa asilimia 70 si sababu ya mkandarasi atumie miezi 10 kukamilisha asilimia 30 iliyobaki. Namweleza mshauri kwa kushirikiana na TARURA (Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini) na Meneja wa Mradi wahakikishe wanafanya tathmini ya kina ya muda ulioombwa ili kupata muda muafaka na kazi iishe mapema," alisema.

Pia aliagiza ifanyike tena tathmini kuangalia namna ya kuhusisha suala la upandaji miti kwenye barabara hizo, na pia vijengwe vibanda vya abiria kwa ajili ya kusubiri usafiri.

Aidha, aliwahakikishia kuwa hati za malipo zote zilizowasilishwa za Sh. bilioni 44 kwa mkandarasi zote zimelipwa.





# RC: Marufuku mawakala ukusanyaji wa mapato

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

SERIKALI mkoani Mbeya, imepiga marufuku halmashauri zote za mkoa huo kuwatumia mawakala kukusanya mapato na badala yake kukusanya zenyewe kwa kutumia maofisa watendaji wa kata.

Mkuu wa Mkoa, Juma Homera, alipiga marufuku hiyo juzi wilayani hapa wakati wa kikao maalumu cha Baraza la Madiwani cha kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema ukusanyaji wa mapato ya serikali kwa kuwatumia mawakala unachangia kuvuja kwa mapato kwa kuwa baadhi ya mawakala wamekuwa wakikusanya fedha hizo na kukaa nazo bila kuziwasilisha halmashauri.

Mkuu huyo wa mkoa alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali pekee, kampuni zilizokuwa zinakusanya mapato zimesababisha upotevu wa zaidi ya Sh. milioni 170 ambazo zilikusanya na kubaki nazo bila kuwasilisha serikalini.

Aliwataka wakurugenzi kusimamia utaratibu huo kwa kuwasimamia maofisa watendaji pamoja na watumishi wengine watakaoaminiwa na kukabidhiwa mashine za kukusanyia mapato hayo.

"Hapa nimeangalia wakala mmoja anadaiwa zaidi ya Sh. milioni 10, mwingine Sh. milioni 12 na mwingine anadaiwa zaidi ya milioni 15 na bado wako wengine. Sasa kuanzia Julai Mosi, mwaka wa fedha utakapokuwa unaanza, ni marufuku mawakala kutumika kwenye ukusanyaji wa mapato," alisema Homera.

Alisema endapo halmashauri zitakusanya zenyewe, kuna uwezekano zikakusanya zaidi ya ambavyo zimekuwa zikiwatumia mawakala na kwamba katika kila halmashauri alizopita alibaini upotevu wa fedha za serikali.

Katika hatua nyingine, Homera aliwapa wiki moja maofisa watendaji wanane wa kata za Wilaya ya Mbarali kurejesha fedha ambazo walikusanya lakini hawakuziwasilisha serikalini ambazo ziko ni zaidi ya Sh. milioni 40.

Pia alitoa siku 10 kwa kampuni ambazo zlipewa tenda ya kukusanya mapato wilayani hapa lakini hazikuziwasilisha serikalini, kuwasilisha fedha hizo kabla hatua kali za kisheria hazijaanza kuchukuliwa dhidi yao.

"Baada ya muda huo kuisha, naliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata na kuwasweka ndani mpaka warejeshe fedha zote walizokusanya na ikiwezekana watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi mpaka fedha hizi zipatikane," alisema Homera.

Aliwaagiza wakurugenzi kuhakikisha wanasimamia vizuri watendaji ili utaratibu wa kukusanya mapato kuanzia Julai, mwaka huu, wawe wanakaa na fedha za serikali.

Awali akitoa taarifa ya ukusanyaji wa mapato wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema halmashauri inategemea zaidi mapato yatokanayo na kilimo cha mpunga, mifugo na shughuli ndogo.

Alisema katika Mwaka wa Fedha 2019/20 halmashauri hiyo ilipanga kukusanya Sh. bilioni 4.6 lakini mpaka kufikia Mei ilikuwa imekusanya Sh. bilioni 4.3 na kwamba mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi huu itakuwa imefikia asilimia 100 za ukusanyaji.

"Huku tunalima zaidi mpunga, tuna viwanda 80 ambavyo vinachakata mpunga, lakini tuna maghala mengi ya kuhifadhia mazao ambayo asilimia 90 ni mpunga," alisema Mfune.



Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Dk. Yahya Msuya (kushoto), akizungumza na wanafunzi wa kike wa Shule ya Msingi Ilindi, kuhusu usafi wa mazingira ikiwamo vyoo vilivyojengwa shuleni hapo na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kupitia mradi wa Sawa. PICHA: NEBART MSOKWA

# DC aitaka taasisi kufanya utafiti udongo

**Na Grace Mwakalinga,**
ILEJE

MKUU wa Wilaya ya Ileje, James Mkude, ameiomba Taasisi ya One Acre Fund, inayojihusisha na utoaji huduma za kilimo na pembejeo, kuanza utafiti wa udongo ili kuwasaidia wakulima kujua aina gani ya mbegu na wakati sahihi wa kulima mazao mbadala kama vile karanga na alizeti ambayo mavuno yake ni mengi ikilinganishwa na mengine.

Mkude alisema hayo jana wakati wa siku ya uvunaji iliyofanyika katika Kata ya Mbebe na kuhudhuriwa na zaidi ya wakulima 220 na viongozi mbalimbali.

Alisema utafiti wa udongo utawasaidia wakulima kulima kwa tija kupitia wataalamu wa kilimo ambao watashauri namna bora ya kulima mazao mbadala ambayo kwa sasa hayajapewa kipaumbele.

"Mazao kama vile karanga na alizeti hapa Ileje yanakubali sana. Nimeona wakulima wanapata mavuno mengi, nashauri tujielekeze huko maana faida ipo, One Acre Fund mtusaidie kutoa elimu ya ugani na masoko ya uhakika, serikali iko nyuma yenu," alisema Mkude.

Mkude aliwahamasisha wakulima kujiunga kwenye vyama vya ushirika ili kuwa na uamuzi wa pamoja katika uuzaji wa mazao yao hususani mahindi ambayo kwa sasa soko lake limedorora. Alimwomba Ofisa Ugani Mkoa wa Songwe kufanya kikao na maofisa ugani wa wilaya zote za Songwe kuweka mikakati ya kutoa elimu juu ya faida za vyama vya ushirika.

Kaimu Mtendaji wa Kijiji cha Mbebe, Mwinuka Mtwangi, alisema mazao ya kimkakati yanafaida kubwa kuliko mazao mengine kama vile mahindi, hivyo aliiomba One Acre Fund kuweka kipaumbele.

Aliongeza kuwa karanga na alizeti kwa debe moja huuzwa kuanzia Sh. 7,000 hadi 8,000 wakati mahindi huuzwa Sh. 4000 kwa debe.

Alisema wateja wa alizeti na karanga ni wa uhakika na kwamba wakiongezewa ujuzi watalima eneo kubwa na kwa ufanisi huku akiomba taasisi hiyo kuendelea kutoa mbegu bora na za uhakika zinazokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

# Wafurahia kuuza mazao kiushirika

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WAKULIMA wa kakao katika Wilaya ya Kyela, wamekiri kuwa utaratibu wa kuuza zao hilo kupitia vyama vya ushirika una tija kuliko utaratibu waliokuwa wanautumia awali ambao ulikuwa unawaumiza.

Wakizungumza na Nipashe juzi, baadhi ya wakulima hao walisema mfumo wa kuuza mazao kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani umewasaidia kupanda kwa bei ya zao hilo kutoka kati ya Sh. 2,000 na 2,500 za awali mpaka Sh. 4,500 na hadi 5,000.

Mmoja wa wakulima hao, Simon Andongolile, kutoka Kanjunjumele alisema mfumo wa awali ulikuwa unaruhusu madalali ambao walikuwa wanawaumiza wakulima na kwamba walikuwa hawana nafasi ya kuonana na wanunuzi moja kwa moja.

Alisema kwa sasa mkulima anauza kakao zake kulingana na bei iliyoko sokoni na akibaini kuwa bei hiyo haina faida kwake anaamua kuacha mpaka itakapotoka bei nzuri.

"Lakini mfumo huu pia unaisaidia serikali kukusanya mapato yake vizuri. Kwa mfano sasa hivi kwa taarifa za mrajis ni kwamba halmashauri yetu imekusanya zaidi ya Sh. milioni 1.3 ambazo awali zilikuwa zinapotea," alisema Andongolile.

Naye Erick Kabombo alisema mfumo wa uuzaji wa zao hilo kupitia vyama vya ushirika imesaidia kuzalisha ajira kwa vijana ambao wanafanya kazi ya kubeba maginia na kuyapanga kwenye maghala.

Alisema awali walikuwa wanauza kakao ikiwa mbichi, hivyo kutengeneza mazingira ya kuwaibia mazao yao kwenye kutokana na vipimo vilivyokuwa vinatumika.

"Pia tunanufaika kupitia vyama vyetu vya ushirika ambapo tunapata bima za afya ambazo zinatusaidia kwenye matibabu mwaka mzima, tunaiomba serikali iendelee kusimamia mfumo huu," alisema Kabombo.

Mrajisi wa Msaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mkoa wa Mbeya, Angela Maganga, alisema zao hilo linalimwa katika halmashauri tatu za mkoa huo ambazo ni Kyela, Rungwe na Busokelo na kwamba mfumo wa ushirika una faida nzuri.

Alisema kwa sasa kakao hizo zinauzwa kwa njia ya mnada ambapo kampuni zinashindanishwa ili kuwawezesha wakulima kupata bei nzuri.

**Alisema kwa sasa mkulima anauza kakao zake kulingana na bei iliyoko sokoni na akibaini kuwa bei hiyo haina faida kwake anaamua kuacha mpaka itakapotoka bei nzuri.**

# Jalada mtuhumiwa ubakaji mtoto kupelekwa kwa DPP

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar linaendelea kumshikilia mtuhumiwa wa ubakaji, Idrisa Juma Pandu, anayetuhumiwa kumwingilia kinyume na maumbile mtoto wa miaka 10.

Mtuhumiwa huyo alikamatwa Juni 12, mwaka huu akimfanyia kitendo hicho mtoto huyo ambaye ni mwanafunzi.

Akizungumza na Nipashe jana Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Awadhi Haji Juma, alisema kuwa polisi inaendelea kufanya uchunguzi na watakapokamilisha upelelezi watapeleka jalada kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa hatua zingine za kisheria.

"Tunashukuru hadi sasa jamii inatupa ushirikiano mzuri kuhusu tukio hili katika kukusanya ushahidi na tutakapokamilisha kazi yetu tutapeleka jalada kwa DPP," alisema.

Alisema matukio hayo ya udhalilishaji yanachangamoto yake kwa baadhi ya jamii yanapotokea kutokuwa tayari kutoa ushirikiano, zinapofikishwa mahakamani wanapohitajika kwenda kutoa ushahidi huwa wagumu.

Alisema licha ya juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na serikali, vitendo hivyo vinaendelea kufanyika na hivi sasa rika kubwa la watoto wanaodhalilishwa ni kuanzia miaka 15 hadi 18.

"Kwa Zanzibar haya matukio ya ubakaji yanaonekana kama vitu vya kawaida japo kuwa hatupendi iwe hivyo...watu utadhani wamelaaniwa kwa sababu kila kukicha huwezi kukosa matukio haya," alisema.

Alisema kuna tukio jingine katika mkoa wake lililoripotiwa wiki iliyopita katika kituo cha Polisi Bububu, mtoto wa miaka 18 wa kike kuingiliwa kinyume na maumbile.

Alisema mtoto huyo amegundulika baada ya wazazi wake kubaini nyendo zake kuwa si nzuri na tukio hilo linadaiwa kufanywa na mwendesha bodaboda kwa madai kuwa mtoto huyoameridhia mwenyewe kutokana na tamaa. Alisema bado kuna kazi kubwa inatakiwa kufanywa na jamii yenyewe na tatizo hilo la udhalilishaji haliwezi kuondoshwa na Jeshi la Polisi pekee kwa sababu matukio hayo bado yanaripotiwa kila siku.

Kamanda huyo alisema kuwa kuna haja ya kufanyiwa marekebisho ya Sheria ya Mtoto kuhusu umri kwa sababu watoto wengi kuanzia miaka 15 ndiyo wamekuwa wakifanyiwa vitendo hivyo kutokana na vishawishi mbalimbali ikiwamo tamaa.

Alisema wasichana wengi wanajihusisha katika vitendo vya ngono kwa kuingiliwa kinyume na maumbile wakihofia kupata mimba na kulinda bikira zao na kuridhia kufanya kinyume na maumbile. "Kwa mujibu wa sheria ni kosa mtu kuingiliwa kinyume na maumbile hivyo anayemwingilia na anayeingiliwa wote wanapaswa kuchukuliwa hatua za kisheria," alisema.

Aliwataka wazazi na walezi kuwa na usimamizi madhubuti wa kuwadhibiti watoto wao na kufuatilia mienendo yao.

Akizungumza kuhusu mtoto wa miaka 10 aliyefanyiwa udhalilishaji Juni 12, mwaka huu, daktari aliyemfanyia uchunguzi mtoto huyo, Fadhil Nassor Hamdu, alisema amempokea mtoto huyo na kumfanyia uchunguzi na alifikishwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, kitengo cha mkono kwa mkono.

"Ni kweli mtoto huyo nimempokea, lakini nilichokigundua baada ya kumfanyia uchunguzi ni siri kwa sababu maadili yetu yanakataza kutangaza siri za mgonjwa wetu...mahakama au Jeshi la Polisi ndiyo lenye mamlaka la kutangaza kuwa mtoto huyo alibakwa au aliingiliwa kinyume na maumbile," alisema.

Alisema kuwa bado udhalilishaji kwa watoto unaripotiwa kituoni hapo na kwa siku hupokea matukio sita ya ubakaji na ulawiti. Kamanda alisisitiza utoaji elimu kwa jamii kuwa watoto wanapofanyiwa vitendo vya ubakaji au ulawiti wasiwasafishe na wawawahishe hospitalini kwa ajili ya uchunguzi.

"Bado uwelewa wa jamii ni mdogo maana watoto wengi wanaofikishwa hapa huwa wameshasafishwa jambo ambalo linaloleta ugumu kumtambua mara moja mfanyaji wa vitendo hivyo," alisema.

Akitoa takwimu za kesi za udhalilishaji kwa Mei mwaka huu, Ramla Hassan Pandu, kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, alisema mwezi Mei, matukio 66 yameripotiwa ikiwamo ya ubakaji 43, ulawiti saba, kutorosha saba na shambulio la aibu tisa.



Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid, akizungumza na Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Mhandisi Zena Ahmed Salum, alipotembelea baraza hilo, Chukwani Zanzibar juzi. PICHA: RAHMA SULEIMAN

## Punguzo bei ya pembejeo za kilimo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa punguzo kubwa ya bei ya pembejeo za kilimo kwa wastani wa asilimia 75 ikiwamo dawa ya kuulia magugu, mbegu, mbolea na huduma za matrekta kwa kilimo cha mpunga ili kuwa na uhakika wa chakula.

Hayo yalielezwa na Waziri wa wizara hiyo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, aliyetaka kujua serikali imejipanga vipi kuondoa tatizo la upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima.

Alisema malalamiko kutoka kwa wakulima kutopata pembejeo kwa kiwango cha kutosha yanatokana na ufinyu wa bajeti inayotolewa na serikali ikilinganishwa na mahitaji halisi.

Alisema mahitaji halisi ya mbolea kwa msimu ni tani 1,800 ya kupandia na 900 ya kukuzia, mbegu bora ni tani 400 na dawa za kuulia magugu lita 30,000.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2020/2021, serikali imenunua mbegu bora tani 50, dawa ya kuulia magugu lita 12,000 na mbolea ya urea tani 244.

Aidha, alisema tani 97 za mbolea ya kupandia, tani 68,45 za mbegu ya mpunga na lita na lita 3,614 za dawa ya kuulia magugu zilizobakia katika msimu wa masika 2019/2020 zimesambazwa kwa wakulima wa mpunga kwa msimu wa vuli 2021 Unguja na Pemba.

# Serikali yajipanga chanjo sahihi Covid-19

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Zanzibar imesema tayari imeshajipanga kwa ajili ya kuwapatia wananchi chanjo sahihi ya Covid-19 wakati wowote zitakapofika Zanzibar.

Mkuu wa Kitengo cha Kudhibiti na Kupambana na Maradhi ya Dharura kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Dk. Hussein Haji, alisema hayo katika kipindi maalumu kinachorushwa na Televisheni ya ZBC jana kwamba matayarisho yote yamekamilika. Alisema wataalamu wa afya wameshaweka mipango pamoja na kutenga vituo maalumu vitakavyotumika huku makundi maalumu ya watakaopaswa kupata chanjo mwanzo yakiwa yameshaandaliwa.

Dk. Hussein alisema tayari wameshafanya utaratibu wa kuweka makundi yatakayopewa kipaumbele ili kurahisisha kazi hiyo katika maeneo yote ya Unguja na Pemba. Alisema pia wameshatenga vituo vya kufanyia kazi hiyo ya chanjo na kuna baadhi ya vituo vitatumika ikiwamo vya kwanza vilivyokuwa vikitumika kwa kupimia Covid-19 na vingine vimetengwa kwa kazi hiyo katika maeneo yote ya Unguja na Pemba.

Alisema kwa kuwa baadhi ya watu wamekuwa na hofu na mitaani kuna maneno mengi yanayosemwa juu ya chanjo hiyo basi jambo la kwanza watahakikisha ni kutoa elimu kupitia vyombo vya habari ili jamii ifahamu umuhimu wa kutumia hiyo chanjo na kuwa ipo salama kwa mwanadamu na haina madhara kama inavyoelezwa katika mitandao ya kijamii.

Mkurugenzi kinga wa Wizara ya Afya, Dk. Fadhil Mohammed, alisema hakuna sababu ya wananchi kuwa na hofu ya matumizi ya chanjo kwa kuwa zipo salama na hakuna madhara makubwa yanayoweza kupata mtu bada ya kuchanja.

Dk. Fadhil alisema wananchi wasiogope chanjo hasa kwa kuzingatia suala la chanjo limekuwa likifanyika mara nyingi, mbali na chanjo ya corona kuna nyingine nyingi wameshatoa kwa wananchi na hawajapata madhara.alisema Dk. Fadhil.

Baadhi ya wananchi wameunga mkono kuletwa kwa chanjo ya corona wakisema ni hatua nzuri kwa kuwa hivi sasa mtu anapotaka kusafiri ni lazima awe na chanjo.

"Mimi siogopi chanjo kwa kuwa mimi ni mfanyabiashara na tunaposafiri tunatakiwa tuwe tumechanja," alisema Asha Hamad Ali.Naye Said Ali Said, alisema ni hatua nzuri kwa serikali kuamua kuleta chanjo kwa kuwa ndiyo hali ya ulimwengu mzima hivi sasa kuchanja wananchi wake ili kujikinga na maradhi hayo, hata hivyo, alisema elimu itasaidia wengi kwa kuwa kuna mambo mengi mitandaoni yanayotia hofu.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, hivi karibuni aliwaambia wananchi kwamba hakuna atakayelazimishwa kuchanjwa kwa kuwa suala hilo linabaki kwenye uamuzi wa mtu mwenyewe.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA YA GHOROFA INAUZWA

Ina frem za biashara, inafaa kwa makazi, au biashara kama Guest house au Hospitali. Ipo Ukonga Dar es salaam. Simu: 0757 079057.

116306601

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI NA 59 YA MWAKA 2021**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**FRANCIS SEMALI MAMBO**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**BERTHA FRANCIS MAMBO**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 5th mwezi JULY 2021

Imewasilishwa Dar Es Salaam leo tarehe …mwezi…mwaka 2016

NAIBU MSAJILI

116313402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**MAOMBI NA: 08/2021**

**OMAR ABDALLAH SUED ……………..MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**AYOUB SADICK SUED NA WENZAKE……..WAJIBU MAOMBI**

**KWA: JAMES KATTO**

**JOSEPH ANDREA BINAMUNGU**
**JUDITH JOHN RUTAMIGWA (POPOTE PALE MLIPO)**

Mnaarifa kuwa Maombi Na. 08/2021 yamepangwa kutajwa tarehe 01/07/2021 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R. Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, mnaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 02/06/2021.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

116313702

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO….OF 20201**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GODFREY JAMES MADEJE**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**DEOGRATIAS GODFREY MADEJE……………………….PETITIONER**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 21/7/2021

Date at Dodoma this 06 Day of APRIL 2021

RESIDENT MAGISTRATE

116313902

---

## TANGAZO LA MNADA

**KESI YA TALAKA NA: 15 YA 2020**
**CESILIA ZAKARIA…..MSHINDA TUZO**
**DHIDI YA**
**EZEKIEL RAPHAEL…MSHINDWA TUZO**

Advanced Credit Recovery Co ltd Kwa amri tuliyopewa na Mahakama ya mwanzo Arusha Mjini, tutauza kwa mnada nyumba iliyoko Sokoni one Mtaa wa Lolovono Wilaya ya Arusha Mjini.

Mnada utafanyika tarehe **30/06/2021** saa 4.00 asubuhi.

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mnunuzi atalipa asilimia **25%** ya bei hapo hapo na asilimia**75%** ilipwe ndani ya siku 14.
2. Nyumba itauzwa kama ilivyo.
3. Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa namba +255767132130, /785132130

**Imetolewa na Dalali wa Mahakama.**

116314002

---

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**AMRI RASHIDI KHAMISI** anatangaza kupotelewa na Hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 262515** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 17/12/2019. Muda wake wa kuisha matumizi ni tarehe 16/12/2029. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Control No. 9910823480239.

115032802

---

**MNADA WA HADHARA**
**KESI NA: 17/2016**
**MDAI-ANNA HAULE**
**DHIDI YA**
**MDAIWA-BLASTON KYANDO**

Kwa idhini tuliyopewa na Mahakama ya hakimu mkazi mfawidhi Mahakama ya wilaya ya Mufindi. Tutauza nyumba moja ambayo iko Mgoloo Kijinini. Mnada utafanyika tarehe 8/7/2021 asubuhi.

**Masharti ya Mnada:**

1. Ukaguzi utafanyika siku tatu kabla ya mnada
2. Mnunuzi atakaeshinda atatakiwa kulipa asilimia 2% (au zaidi) mara tu baada ya kushinda na salio lililobaki atatakiwa kumalizia ndani ya siku 14 tangu tarehe ya mnada.
3. Endapo mshindi atashindwa kulipa ndani ya muda uliotolewa atakuwa amepoteza haki yake na mali itauzwa upya.

**Kwa Mawasiliano piga no:**
**0767 969133/0655 969134/0769 848485**
**Majembe Auction Mart- Iringa.**

116313602

---

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD,** Sepco na MM tutauza kwa mnada wa hadhara Mali za wadaiwa Sugu kama ilivyotangazwa

| Mdaiwa/ mdhamini | Dalali | Aina ya Mali/ Mahali | Tarehe mnada |
|---|---|---|---|
| AMINA MARTIN BAGULE (MARY HARRIETH CHIBIBI LONGWAY) | **SEPCO** Debt Collection & Auctioneering Co. Ltd | Gari - Toyota land Cruiser T.297 ASV, Makumbusho Yard-Dar | 2.07.2021 |
| ALFRED ASAJILE KANDONGA | MM Auctioneer & Debt Collector Co. Ltd | Kiwanja- Kahama Ilemela Mwanza | 3/07/2021 |

Minada yote itafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**SEPCO - 0715683777/0712670704**
**MM -0784784456/0768990064**

116314302

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PHILIPO HOSIANA MAHENGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya NISSAN X-TRAIL yenye namba za usajili T220 CBT engine namba QR20034090A chasisi namba NT30018176,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochocte cha polisi

**Polisi taarifa MKB/R-B/107/2021**






**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

## OFISI ZA MATANGAZO

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA

# Mwalimu mwenye ulemavu azawadiwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, ametoa Sh. 50,000, kiti na meza kwa mwalimu mwenye ulemavu wa miguu katika Shule ya Sekondari Ngokolo, Ernest Mpanda, kwa kufanikisha matokeo mazuri kidato cha nne mwaka 2020.

Mwalimu huyo amesaidia kupunguza daraja 'F' katika matokeo ya mtihani kidato cha nne 2020.

Mboneko alitoa zawadi hizo juzi wakati akikabidhi meza 12 na viti viwili, kwa ajili ya matumizi ya walimu katika shule hiyo.

Kabla ya kukabidhiwa vifaa hivyo walikuwa wanatumia vya wanafunzi wanavyotumia kukalia darasani.

Alisema alifikia uamuzi huo wa kumkabidhi zawadi hizo kutokana na juhudi zake ambazo anazifanya huku akiahidi kuendelea kutatua kero za walimu wenye ulemavu wilayani humo.

Miongoni mwa kero hizo ni pamoja na kuwajengea mazingira rafiki ya kufundishia na miundombinu ya choo.

"Nimefurahishwa sana na mwalimu huyu kwa kufundisha vizuri wanafunzi na kupunguza daraja la F shuleni hapa nina imani katika matokeo ya kidato cha nne 2021, hakutakuwa na F kabisa," alisema Mboneko.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Ngokolo, Malale Masali, alisema licha ya hali ya ulemavu ya mwalimu hiyo, amekuwa mkombozi shuleni hapo kwa kuhakikisha wanafunzi wanapata ufaulu wa daraja la juu.

Alisema katika matokeo ya kidato cha nne mwaka 2019, kulikuwa na 'F' 23 shuleni hapo, lakini mwalimu huyo alipambana kufundisha na kuzipunguza hadi kufikia tisa.

Naye Makamu Mwenyekiti wa bodi ya shule hiyo, Eliaremisa Mbise, aliwataka wazazi kutowabeza watoto wenye ulemavu na kuwaficha ndani badala yake wawapeleke shule ili watimize ndoto zao.

Kwa upande wake, mwalimu Ernest, alimpongeza Mkuu wa wilaya kwa kuwajali walimu wenye ulemavu na kuahidi kutomwangusha kwa kuhakikisha anaifuta 'F' shuleni hapo.

# Hivi ndivyo kodi laini za simu itakavyotozwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amelazimika kutoa ufafanuzi kuhusu makato ya kodi kupitia miamala ya simu, huku akiweka wazi kuwa mtumiaji atakatwa mara moja kwa vocha atakayoweka na si kwa simu kama inavyodaiwa.

Mwigulu alilazimika kutoa ufafanuzi huo jana kwenye Mkutano wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Taasisi zake na Waharqiri wa Vyombo vya Habari jijini hapa.

Alisema kuanzia Sh. 100,000 kwenda juu anatozwa Sh. 200 na sio kila siku, na ni pale anapoweka, Sh. 0,000 hadi 100,000 anatozwa Sh. 180 huku, Sh.2,500-5,000 atatozwa Sh. 21.

"Kia mfano, mimi kwenye laini yangu ya Halotel kuna kifurushi kinaitwa Tanzanite unaipa Sh. 50,000 kwa mwezi maana yake kwenye kiasi hicho kwa mwezi nitakatwa Sh. 180. Hivi kwa vifo vya mama zetu mtu unayeweka 50,000 ukatozwa hiyo fedha kuokoa maisha yao kwenye kuboresha huduma kuna shida gani, nikaweka TTCL wakanitoza Sh. 100 kwa mwezi."

"Nimeona watu wanachanganya hata kule bungeni wanasema sasa kila siku itakuwa inakatwa Sh. 10 hadi 200 kila siku, wanasema hata kama hukuweka vocha inakuwa kama ile ya nipige tafu, hatukuweka hivyo na wala hatujaweka Sim Card Tax, tulichoweka ule ni uwiano tu tunasema kwa mtu ambaye anaweka kuanzia Sh. 1,000 hadi 2,500 pale anapoweka ndio anatozwa Sh. 10, inayotajwa ni Sh. 200 inaonekana bibi wa kijijini huko anakwenda kukatwa Sh. 200, sio kweli," alisema.

Waziri huyo alisema makato hayo ni pale mtu anapoweka vocha sio kama anavyopiga.

Kuhusu miamala ya kutuma fedha, Mwigulu alisema kwa Sh. 1,000 hadi 2,000 atatozwa Sh. 10, Sh. 10,000 hadi 15,000 anatozwa Sh.300 kwa muamala wa Sh.30,000 na kuendelea atatozwa Sh.1,000 huku kuanzia Sh. milioni tano na kuendelea atatozwa Sh. 10,000.

"Sio kwamba Sh. 10 ni mzigo na sio kwamba siwahurumii Watanzania, lakini tukapima shida walizo nazo Watanzania, maendeleo ya nchi yetu yatajengwa na Watanzania wenyewe," alisema.

Kuhusu mfumo wa ulipaji kodi, alisema kuna maeneo kuna shida na kwamba kwa miaka yote walipakodi waliosajiliwa wapo chini ya milioni tatu na walipakodi wakubwa wapo kati ya 400-500.

"Hatukimbilii kupandisha kodi kwa kuwa kodi zingine zinaua ajira na kukimbiza wawekezaji na kuua sekta binafsi, kuna miradi mikubwa inahitaji fedha tutawaunganisha wapi Watanzania pamoja, wakiwa wengi tunapunguza mzigo, tunagawanya huu mzigo hili jukumu ni la Watanzania wenyewe," alisema.

Akizungumzia makato ya Sh. 100 kwa lita ya mafuta ya petroli na dizeli, Mwigulu alisema kodi hiyo ambayo imeongezeka serikali itapeleka fedha hizo kama ilivyoeleza kwenye bajeti kwamba zitapelekwa TARURA kwa ajili ya ujenzi wa barabara ambazo nyingi ni mbovu na kusababisha adha kubwa kwa wananchi ambao wanahitaji huduma mbalimbali za kijamii.




Mkuu wa Wilaya Temeke, Godwin Gondwe (katikati), akishukuru baada ya kupokea mabati 576 yaliyotolewa na Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard (mwenye tai), kwa ajili ya shule za msingi za Yombo Dovya, Tuangoma na Faraja, katika hafla iliyofanyika wilayani humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ibada ya hija yafutwa kisa corona

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI ya Saudi Arabia, imefuta ibada ya hija kwa mwaka huu kwa mahujaji kutoka nje ya nchi hiyo kutokana na ugonjwa wa corona.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mufti wa Tanzania, Sheikh Mkuu Abubakar Zubeir bin Ally, kwa waandishi wa habari jana, Dar es Salaam, ibada hiyo itatekelezwa kwa raia wa Saudi Arabia pekee na si wananchi kutoka katika mataifa mengine duniani.

"Hakutokuwa na hija mwaka huu, isipokuwa itatekelezwa na wenyeji wa nchi ya Saudi Arabia pekee pamoja na wageni ambao ni wakazi wa nchi hiyo na ni kutokana na matatizo haya ya ugonjwa wa corona.

"Serikali ya Saudi Arabia kupitia wizara yake ya hija wameona mwaka huu waifute hija kwa watu kutoka katika nchi za nje na ibakie kwa wenyeji peke yake, tena kwa idadi ndogo ya mahujaji elfu 60 tu," alisema na kuongeza:

"Kuna chombo kinaundwa katika nchi ile kwa utaratibu wa Saudi Arabia wa Wizara ya hija, inaitwa Haji Mission ambayo na Tanzania tunayo inayoitwa Tanzania Haji Mission, ambayo ndiyo inashughulika na mambo ya hija tu. Kwa hiyo sisi kama Baraza tunaimonitor hiyo katika kuendesha masuala ya hija.

"Na taasisi zote zinakuwa ziko chini ya uangalizi wa hiyo Tanzania Haji Mission. Tunaamini kwamba waliolipa kwa ajili ya hija ni lazima watakuwapo kwa sababu tayari watu wanaendelea kujiandaa na wengine kipindi hiki ndio wanakuwa wanamiminika kwa masuala hayo ya hija."

Mufti Zubeir alisema kwa ambao watakuwa wamelipia kwa ajili ya hija utaratibu kuhusu pesa zao utatangazwa baaadye na taasisi hiyo ya Tanzania Haji Mission.

"Kwa hiyo kutakuwa na utaratibu maalum ambao utatangazwa na kuelezwa na hii Tanzania Haji Mission juu ya namna gani walilipa kama watarudishiwa pesa zao au zitawekwa kwa ajili ya mwakani.

"Na sisi tunazidi kutoa rai kwamba ni vizuri kutokuchukua pesa zao, wangejaribu kuzibakisha katika taasisi ambazo wamelipia kwa ajili ya mwakani. Swali sasa litakuja sasa je, nikifa, ukifa si una warithi... warithi watakuja kuangalia namna gani itakavyokuwa, lakini maelezo makubwa juu ya suala hilo yataelezwa na kile chombo chetu kinachoitwa Tanzania Haji Mission," alisema.

Ni mara ya pili sasa kuahirishwa kwa ibada hiyo ya hija kutokana na janga la corona na mara ya kwanza ilikuwa mwaka jana.



# POGBA ALALAMA RUDIGER KUMNG'ATA MGONGONI

**MUNICH, Ujerumani**

PAUL Pogba amedai Antonio Rudiger "alimng'ata" yeye wakati Ufaransa ikiibuka na ushindi dhidi ya Ujerumani kwenye michuano ya Euro 2020, lakini hataki mlinzi huyo afungiwe kwa kitendo hicho.

Kiungo huyo wa Manchester United alionekana mwenye hasira kali baada ya Rudiger kuonekana kwenye camera akisogeza uso kwenye mgongo wa Pogba kabla ya mikono yake kufikia kifuani kwa Mfaransa huyo.

Pogba alionekana kumwambia mwamuzi kwamba, Rudiger alimng'ata baada ya kipindi cha kwanza cha mchezo huo uliopigwa hapa Munich.

"Sililii kadi, njano au nyekundu kwa sababu ya tukio hilo," alisema Pogba.

"Alining'ata, nafikiri ni kidogo. Lakini tumejuana mimi na yeye kwa muda mrefu sana.

"Nilimwambia mwamuzi na alichukua hatua. Imeshaisha hiyo.

"Ilikuwa mechi kubwa kwa upande wetu ... na sikutaka yeye afungiwe kwa hali ile. Na mwisho wa mchezo tulikumbatia na ni hivyo tu."

Ufaransa walipoteza mchezo huo wa Kundi F kwa kichapo cha bao moja ambalo mlinzi wake, Mats Hummels alijifunga akiwa kwenye harakati za kukoa hatari.

## MAN CITY KUANZIA SPURS EPL 2021-22

**LONDON, England**

MANCHESTER City itaanza kutetea taji la Ligi Kuu England kwa kucheza na Tottenham Hotspur.

Kikosi hicho cha Pep Guardiola ambacho kilishinda taji hilo msimu uliopita wa 2020-21, kitaanza kampeni yake pale kwenye dimba la Tottenham Hotspur Agosti 14, mwaka huu.

Hii ni kwa mujibu wa ratiba ya Ligi Kuu ya England ambayo ilitoka rasmi jana.

Chelsea ambao waliwafunga Man City bao 1-0 na kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakiwa chini ya kocha, Thomas Tuchel, wao wataanza ligi kwa kucheza na Crystal Palace.

Manchester United ambao walishika nafasi ya pili wakiwa na kocha, Ole Gunnar Solskjaer wataanza msimu mpya wa kucheza na kikosi cha kocha, Marcelo Bielsa, Leeds pale kwenye dimba la Old Trafford.

Waliopanda daraja, Brentford wataanza ligi kwa kucheza na Arsenal, ambao hawajafuzu kucheza mashindano ya Ulaya kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 1995-96.

Liverpool wataanza na Norwich iliyopanda daraja, huku Watford akicheza na Aston Villa.


Mechi zote za ufunguzi wa Ligi hiyo msimu wa 2021/22 Agosti 14 ni: Brentford vs Arsenal, Burnley vs Brighton, Chelsea vs Crystal, Everton vs Southampton, Leicester vs Wolverhampton, Man United vs Leeds, Newcastle vs West Ham,

Norwich City vs Liverpool, Tottenham vs Man City na

Watford vs Aston Villa

## MORATA YUPO SANA JUVENTUS

**TURIN, Italia**



ALVARO Morata atatumia msimu mwingine na Juventus baada ya miamba hao wa Serie A kuongeza mkataba wake wa mkopo hadi Juni 30, 2022.

Straika huyo amekubali kubaki Turin, ambako alitumia msimu wa 2020-21 akicheza kwa mkopo akitokea Atletico Madrid.

Morata alifunga mabao 20 kwenye mashindano yote msimu uliopita, ikiwa ni msimu bora zaidi kwake katika mashindano yote, huku akitoa pasi za mwisho 11.

Juve ilisema katika taarifa yake Jana: "Morata atabaki na sisi na huu ni wakati muafaka kwa kukaa tena kwa mwaka mmoja!"

Morata alitumia miaka miwili pale Juve kutoka msimu wa 2014 hadi 2016 kabla ya kurudi Real Madrid kwa msimu wa 2016-17.

Baada ya kuwa na msimu mgumu kule Chelsea, alihamia Atletico awali kwa mkopo mwaka 2019 kabla ya kusaini mkataba wa kudumu mwaka mmoja baadaye.

Kwa ujumla, Morata amefunga mabao 47 na pasi za mwisho 27 katika mechi 79 alizoanza na 'Bianconeri' hao kwenye mashindano yote.

## HABARI MICHEZO

# ARSENAL YAELEKEZA RADA BUNDESLIGA

**LONDON, England**

ARSENAL wameripotiwa kuwa katika mchakato wa kutazama namna ya kumnasa mchezaji wa RB Leipzig, Tyler Adams msimu huu wa majira ya joto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, alifanya vema akiwa na klabu yake hiyo ya Bundesliga wakati wa msimu wa 2020-21, akicheza mechi 37 kwenye mashindano yote, na kuchangia bao moja na pasi moja ya mwisho katika mchakato huo.

Kwa mujibu wa The Athletic, Arsenal imevutiwa na uwezo wa Adams, na 'Washikabunduki' hao wanaangalia uwezekano wa uhamisho wake kwa msimu huu wa usajili wa majira ya joto.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Marekani alicheza sana kama kiungo wa kujihami na klabu yake msimu uliopita, lakini alitumika kama kiungo wa kulia na beki wa kulia.

Leipzig wana nafasi nzuri ya kumbakiza mchezaji huyo, kwani Adams ana mkataba hadi msimu wa 2024-25.

Adams amecheza mechi 66 akiwa na RBL tangu kuwasili kwake kutoka New York Red Bulls mwaka 2019.

# UNITED YAMGEUKIA NAVAS WA PSG

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United wanafuatilia kwa karibu hali ya golikipa, Keylor Navas huko Paris Saint-Germain, kwa mujibu wa ripoti.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Costa Rica, ametumia misimu miwili iliyopita kama kipa chaguo la kwanza la PSG, akicheza mechi 80 za wababe hao wa Ligue 1.

Hata hivyo, timu hiyo ya Ufaransa inatarajiwa kutangaza hivi karibuni kusainiwa kwa golikipa wa AC Milan, Gianluigi Donnarumma kwa uhamisho huru.

Chanzo cha habari kutoka Hispania, kimeliambia Marca kwamba, Navas hatakuwa na budi kusaka kuondoka hapo Parc des Princes mara tu Donnarumma atakapofika kwani hayuko tayari kucheza kama chaguo la pili.

Na Man United wanasemekana ni mojawapo kati ya timu tatu zinazovutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, pamoja na wenzao wa Serie A, Juventus.

Navas, ambaye hapo awali alikuwa kwenye klabu ya Real Madrid kwa misimu mitano, alisaini nyongeza mpya ya mkataba wa miaka mitatu na PSG, Aprili mwaka huu.





# ABRAMOVICH

## AFUNGIA KAZI USAJILI HALAAND

**LONDON, England**

MMILIKI wa Chelsea, Roman Abramovich, anaonekana amedhamiria kumsajili nyota wa Borussia Dortmund, Erling Halaand kipindi hiki cha majira ya joto.

'The Blues' hao wamekuwa wakimwinda mshambuliaji huyo na sasa Abramovich ametenga kiasi cha pauni milioni 154. 5.

Bilionea huyo wa Urusi msimu uliopita wa kiangazi alifanya usajili wa majina makubwa, na sasa yuko tayari kutumia fedha nyingi msimu huu wa majira ya joto ili kuifanya timu hiyo iweze kutoa changamoto kwa taji la Ligi Kuu msimu ujao.

Chelsea msimu huu ulikuwa bora sana kwao kwa kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini kwenye ligi walimaliza nafasi ya tatu.

Wiki hii mambo yamepamba moto katika shughuli za usajili huku vyanzo vyote vya soka vikiripoti tetesi hiyo.

Hata hivyo, dau la kumng'oa mchezaji huyo halitakuwa dogo, lakini kulingana na jarida la Marca, Abramovich yupo tayari kulipa dau hilo la pauni milioni 154.5.

Mmiliki huyo wa The Blues yuko tayari kulipa kiasi hicho hata zaidi ili kuhakikisha tu nyota huyo hatui jijini London kwa ajili ya msimu ujao.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO AVUNJA REKODI MABAO MICHUANO EURO

## Ni ile iliyowekwa na Michael Platini mwaka 1984, sasa aitafuta ya...

**BUDAPEST,** Hungary

CRISTIANO Ronaldo amevunja rekodi baada ya kuwa mchezaji anayeongoza kwa kufunga mabao kwenye historia ya michuano ya Mataifa ya Ulaya.

Ronaldo alifunga mara mbili wakati Ureno wakishinda 3-0 dhidi ya Hungary na kumfanya afikishe mabao 11 kwenye michuano ya Euro.

Na sasa amempiku gwiji wa Ufaransa, Michael Platini, ambaye alifunga mabao tisa katika mechi tano za michuano ya Euro 1984.

**Mshambuliaji huyo wa Juventus pia amekuwa mchezaji wa kwanza kucheza michuano mitano tofauti ya Euro na pia kuwa mchezaji wa kwanza kufunga kwenye michuano mitano mfululizo.**

Awali ilionekana kama ni usiku ngumu kwa Ronaldo pale Budapest, Hungary hadi Raphael Guerreiro alipoifungia bao la kwanza Ureno dakika ya 84.

Na nahodha wa Ureno, Ronaldo akafunga la pili dakika ya 87 kwa mkwaju wa penalti, kabla ya kufunga la tatu dakika tano baadaye.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Ronaldo kucheza mashindano hayo tangu alipoumia kwenye fainali ya mashindano hayo mwaka 2016 dhidi ya Ufaransa na walibuka mabingwa.

Pia, ameweka rekodi nyingine ya kucheza mechi 22 katika mashindano hayo ya Euro. Mabao yake mawili dhidi ya Hungary yamemfanya apitwe bao moja tu na Miroslav Klose (aliyefunga 19) kwa mchezaji wa Ulaya katika mashindano ya Dunia na Euro.

Na sasa Ronaldo amebakiwa na mabao matatu tu kuifikia rekodi ya Ali Daei (aliyefunga mabao 109) kwenye mechi za kimataifa.

Raia huyo wa Iran alifunga mabao hayo kwa kipindi cha miaka 13 aliyocheza tangu mwaka 1993.

## KWA UFUPI

### STERLING KUBAKI MAN CITY
WINGA wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 26, anatarajiwa kubaki Manchester City msimu ujao, licha ya kuhusishwa kwake kutaka kuondoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu England. (***Manchester Evening News***)

### SILVA ANATAKA KUONDOKA
KIUNGO wa Manchester City, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 26, angependelea kutimka msimu huu, lakini kocha Pep Guardiola amegoma kumruhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno kuondoka. (***Athletic***)

### RONALDO, POGBA KUPISHANA
MANCHESTER imetoa ofa ya pauni milioni 17 kwa ajili ya kumrejesha mshambuliaji wake wa zamani, Cristiano Ronaldo kutoka Juventus, katika mpango ambao utashuhudia kiungo Mfaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28, akienda upande wa pili. Hata hivyo, chaguo la Ronaldo ni klabu ya Paris St-Germain. (***Gazzetta dello Sport, via Mail***)

### RAMSEY NJIAPANDA JUVE
JUVENTUS inatarajiwa kufanya mazungumzo na wawakilishi wa kiungo, Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 30, kujaribu kutafuta namna ya kuachana na nyota huyo wa kimataifa wa Wales. (***Goal***)

### OUSMANE KUONGEZA MKATABA
BARCELONA imefanya mazungumzo na wawakilishi wa mshambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele, kuhusu kumwongezea mkataba nyota huyo mwenye umri wa miaka 24, lakini hakuna hatua yoyote iliyopigwa katika kikao cha kwanza. (***Marca***)

### ARSENAL WANAMTAKA ONANA
ARSENAL wanamwangalia golikipa wa Ajax, Andre Onana mwenye umri wa miaka 25, lakini bado hawajapeleka 'ofa' yoyote kwa raia huyo wa Cameroon anayetumikia adhabu ya kufungiwa miezi tisa. (***Goal***)

### ARSENAL WAGOMEWA LOKONGA
KLABU ya Anderlecht imekataa dau la pauni milioni 13.5 kutoka Arsenal kwa ajili ya kumuuza kiungo wao kinda, Albert Sambi Lokonga mwenye umri wa miaka 21, kwani wanataka pauni milioni 18. (***Mail***)

### WELBECK NA MKATABA
KLABU ya Brighton inataka kumwongezea mkataba mshambuliaji, Danny Welbeck mwenye umri wa miaka 30. (***Brighton Argus***)

### COMAN KUBAKI BAYERN
WINGA wa Ufaransa, Kingsley Coman mwenye umri wa miaka 25, ambaye anahusishwa kutaka kuhamia Manchester United, hatarajiwi kuondoka Bayern Munich kwani yuko kwenye mipango ya kocha Julian Nagelsmann 25. (***Goal***)

### SERGIO AKATALIWA SEVILLA
MKURUGENZI wa michezo wa Sevilla, Monchi amepuuzia tetesi kwamba, mlinzi wa kati wa Hispania, Sergio Ramos atarejea klabuni hapo na kusema anafikiri mkongwe huyo mwenye umri wa miaka 35 yuko kwenye mazungumzo na klabu yake ya Real Madrid ili kusalia klabuni hapo. (***Sky Italia, via Marca***)

### PARKER KUONDOKA FULHAM
KOCHA wa Fulham, Scott Parker anatarajiwa kuikacha klabu hiyo wiki hii huku Bournemouth ikimtaka kwa udi na uvumba ili awe kocha wao mpya. (***Telegraph***)

HABARI MICHEZO

# YANGA NA MBIO ZA UBINGWA, RUVU SHOOTING KULIPA KISASI

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikihitaji kupata pointi tatu leo ili kuendelea kumkimbiza kinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, katika mbio za ubingwa, wapinzani wao, Ruvu Shooting wamepania kuhakikisha wanalipa kisasi cha kupoteza dhidi yao kwenye mzunguko wa kwanza.

Timu hizo zitashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa leo kuvaana kwenye mechi ya raundi ya pili, Ruvu Shooting ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza mzunguko wa kwanza kwa mabao 2-1. Licha ya kuzidiwa alama sita na vinara Simba, Yanga inaamini watani wao hao wanaweza kupoteza baadhi ya mechi zao, hivyo wana kila sababu ya kushinda michezo yao mitano iliyosalia, ikianza na ya leo dhidi ya Ruvu Shooting.

Yanga ambayo inafundishwa na Kocha Mkuu, Mtunisia Nasreddine Nabi, huku Ruvu Shooting ikinolewa na mzawa, Boniface Mkwassa, ambaye aliwahi kuichezea pamoja na kuwanoa Wanajangwani hao, leo wataziongoza timu zao dimbani kila mmoja akiwa na malengo tofauti.

Kocha wa Makipa wa Yanga, Razak Siwa, aliliambia gazeti hili kuwa mapumziko ya wiki mbili waliyopata wakati ligi imesimama kupisha mechi za kirafiki za kimataifa za timu za taifa, yamesaidia kuwapa maandalizi mazuri na bado wana matumaini ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu.

Alisema wamejiandaa vizuri kwa kufanyia kazi upungufu uliojitokeza katika mechi zilizopita ikiwamo safu ya ushambuliaji kwa kuitaka kuwa makini kwa nafasi wanazotengeneza uwanjani.

"Mapumziko yametusaidia kufanya maboresho katika upungufu uliopo katika kikosi chetu, nina imani mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu tunahitaji pointi tatu muhimu ili tujiweke katika mazingira mazuri ya mbio zetu za kuwania ubingwa.

"Huu ni mpira, tunawaheshimu na tumejiandaa vizuri kwa ajili ya mechi yetu dhidi ya Ruvu Shooting na mashabiki wa Yanga wafike uwanjani ili kupata burudani na kuondoka na pointi tatu muhimu," alisema Siwa.

**Nahodha msaidizi wa Yanga, Ramadhani Kabwili, alisema malengo yao makubwa ni kufanya vizuri katika kila mechi ikiwamo dhidi ya Ruvu Shooting kuhakikisha wanapata pointi tatu muhimu.**

Alisema mechi hiyo itakuwa ngumu kwa kuwa kocha wa wapinzani wao (Mkwassa), anawafahamu vizuri kwa kutokana na kuwahi kuifundisha timu hiyo tena kwa kipindi cha hivi karibuni.

"Tunaenda kwa kuwaheshimu sana wapinzani wetu hao, kwa sababu wametoka kupoteza mechi yao ya mwisho na kocha wao naye anaijua vizuri timu yetu kwa sababu baadhi ya wachezaji walikuwapo wamewahi kutoka katika mikono ya Mkwassa," alisema Kabwila.

Kocha Msaidizi wa Ruvu Shooting, Rajab Mohamed, kwa upande wake, alisema wamejiandaa vizuri na wanaiheshimu Yanga, lakini watahakikisha wanapambana katika mchezo huo kulipa kisasi.

Alisema mechi ya awali walipoteza kwa mabao 2-1, hivyo wamejiandaa vizuri kwa ajili ya kulipa kisasi katika mchezo huo ambao anaamini utakuwa na ushindani mkubwa.

"Tunawakosa Abdulrahaman Mussa, Juma Nyosso na Abdallah Rashid, lakini kutokuwapo kwao hakutaathiri mipango yetu kwa sababu tayari watu wameandaliwa kuchukuwa nafasi zao na tutafanya vizuri katika mechi yetu hiyo dhidi ya Yanga," alisema Mohamed.

MCHUJO...




Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Benjamin Kalume (katikati), akitangaza majina yaliyopita katika mchujo wa awali wa wagombea wa nafasi mbalimbali katika shirikisho hilo jana jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mkurugenzi wa Sheria, Habari na Masoko wa TFF, Boniface Wambura na Mwanasheria wa shirikisho hilo, Rahimu Shabani. **MPIGAPICHA**

# 22BET yawawezesha wenye 'vibanda umiza'

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI inayojihusisha na michezo ya kubahatisha ya 22BET, imetoa msaada wa kuboresha mazingira ya vibanda vinavyoonyesha mpira maarufu kama 'vibanda umiza', katika mitaaa ya Wilaya za Kinondoni na Ubungo, Dar es Salaam.

Baadhi ya vitu vilivyowasilishwa na kampuni hiyo jana ni pamoja na mbao za kisasa za kuandikia matangazo ya mpira, mabango na vifaa vya kujilinda dhidi ya virusi vya corona vikiwamo barakoa.

Ofisa Uhusiano kwa Umma wa Kampuni hiyo, Mored Kaisi, aliwaambia waandishi wa habari kuwa wamechukua hatua hiyo kwa lengo la kuunga juhudi za kutanua wigo wa ajira kwa Watanzania, kuweka mazingira bora kwa wapenzi wa michezo na kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika mijadala ya michezo. "Tumepita kwenye 'vibanda umiza' takriban 50 hadi sasa, tukishirikiana nao katika kuboresha maeneo yao ya kuonyesha mpira pamoja na kuwapa baadhi ya vitendea kazi. Tunaamini mashabiki wengi wa kweli wa soka wanakutana katika maeneo haya," Kaisi aliwaambia waandishi wa habari.

"Tumeamua kuongeza ushirikiano na wenzetu wa vibanda umiza ili kurejesha kwa jamii na kushiriki katika kuboresha maisha yao. Burudani hizi ni sehemu ya ajira kwa watu wengi. Na sisi kama kampuni tunaunga mkono juhudi za kuongeza wigo wa ajira rasmi na zisizo rasmi," aliongeza.

Aidha, ofisa huyo alisema wamechagua kuanza na wakati huu ili kutoa fursa bora zaidi kwa wapenzi wa soka kufuatilia Michuano ya Euro 2020 inayoendelea katika miji mbalimbali barani Ulaya, wakiwa katika mazingira bora zaidi. Pia michuano ya soka inayoendelea hapa nchini.

Mmoja kati ya wamiliki wa vibanda umiza, katika eneo la Manzese, Nasibu Ramadhani, aliishukuru kampuni hiyo kwa kuwakumbuka na kuwapa msaada. Alisema msaada huo utasaidia kuongeza mvuto wa biashara zao, kwani wateja wengi watajisikia wako salama zaidi wanapokutana kushuhudia mitanange hiyo.

## Diwani Tabata ageukia michezo

**Na Shufaa Lyimo**

DIWANI wa Kata ya Tabata jijini Dar es Salaam, Omary Abdallah Matulanga, ameikabidhi timu ya Umoja Road Veterani, vifaa vya michezo vyenye thamani ya shilingi 230,000 kwa ajili ya kuipa nguvu timu hiyo.

Akizungumza na viongozi wa timu hiyo ofisini kwake baada ya kukabidhi vifaa hivyo, aliwataka kuandaa katiba ambayo wataipeleka Baraza la Michezo Tanzania (BMT), ili kupata kusajili.

"Ninaomba muandae katiba mwipeleke BMT ili mpate mwongozo wa kusajili klabu yenu nipo tayari kugharamia gharama zote ambazo zitahitajika kwa ajili ya kuisajili klabu yetu itambulike kisheria kwa sababu natambua faida ya michezo," Matulanga alisema huku akiahidi kuendelea kushirikiana nao bega kwa bega.

Alisema bado ataendelea kutoa vifaa vingine vya michezo ambavyo anatarajia kuvitoa hivi karibuni akiamini michezo inajenga afya na kuwataka vijana hao kupenda kushiriki mazoezi mara kwa mara kwa ajili ya kujenga mwili yao.

Kwa upande wa Katibu Mkuu wa timu hiyo, Makata Dutch, alimshukuru kiongozi huyo kwa kuamua kuwapa vifaa vya michezo na kuahidi kufanya juhudi ya kuandaa katiba haraka ili wapate usajili.

## Biashara yafurahia sare kwa Namungo

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Biashara United, umeeleza kufurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wao katika mchezo wa juzi, ambao walikutana na timu ya Namungo FC na kupata matokeo ya kufungana bao 1-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Klabu hiyo, Patrick Odhiambo, alisema vijana wake wamejitahidi kupata pointi moja wakiwa kwenye uwanja wao wa nyumbani licha ya kuwa mchezo ulikuwa na ushindani mkali.

"Mchezo ulikuwa na ushindani lakini wachezaji wangu wamejituma tukafanikiwa kupata pointi moja, makosa madogo madogo ambayo nimeyaona nitayafanyia kazi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo mmoja kabla ya kwenda Tabora kukutana na Yanga kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la Azam," alisema Odhiambo.

Biashara ambayo sasa imefikisha pointi 46 baada ya michezo 31, ikiwa nafasi ya nne, Jumapili itashuka dimbani kuikaribisha JKT Tanzania. Kwa upande wa Namungo yenyewe ina pointi 42 katika nafasi ya tano kutokana na kushuka dimbani mara 31.

# Michezo

Alhamisi Juni 17, 2021
Nipashe



POGBA ALALAMA RUDIGER KUMNG'ATA MGONGONI HABARI UK 20

## LA TATU HILO...



Mshambuliaji wa Ureno, Christiano Ronaldo akiifungia timu yake bao la tatu wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Hungary kwenye mechi ya michuano ya Euro 2020 iliyopigwa Uwanja wa Ferenc Puskas mjini Budapest, Hungary juzi. **PICHA: MTANDAO**

## YANGA: TUTACHEZA NA SIMBA JULAI 3

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema itakwenda uwanjani kucheza mechi yao dhidi ya Simba iliyopangwa kupigwa Julai 3, mwaka huu, kama ilivyokubaliana na serikali, Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi.

Kaimu Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Haji Mfikirwa alisema hakuna sehemu yoyote ambayo klabu yao imetoa taarifa kuwa haitopeleka timu uwanjani kama inavyosemwa na baadhi ya watu ambao si viongozi.

Kaimu Katibu mkuu huyo alisema hayo kufuatia wazee wa klabu hiyo waliojinasibu kuwa ni Baraza la Wazee wa Yanga kufanya mkutano kwenye klabu hiyo na kudai kuwa timu haitokwenda kucheza mechi baina yao ya Simba.

"Walichokieleza ni maoni yao, lakini si msimamo rasmi wa klabu. Klabu ya Yanga ina utaratibu wake wa kutoka tamko au taarifa rasmi na anayetakiwa kufanya hivyo ni Mwenyekiti, Katibu Mkuu na Msemaji wa Klabu na si mtu mwingine yoyote," alisema Mfikiriwa.

Kuhusu kutumia klabu kuelezea jambo hilo, ikiwamo nembo za wadhamini, Kaimu Katibu Mkuu alisema kuwa wazee hao waliomba kuongea, na wao waliwakubalia kama wazee, lakini jambo walilokwenda kuongea, wakaongeza na mengine ambayo hayakuwamo.

# KIVUMBI PANGA UCHAGUZI TFF

## ●●●Mayay kutema nyongo leo, Karia, Hawa na Mgeusa wapeta mchujo urais, pingamizi zakaribishwa kuanzia Juni 19 hadi...

**Na Saada Akida**

KIVUMBI cha kukubali matokeo ama kupinga panga la mchujo wa kuwania nafasi mbalimbali katika Uchaguzi Mkuu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), nafasi ya urais na wajumbe wa kamati ya utendaji, kinatarajiwa kujulikana leo baada ya waliopenya na waliokatwa kutangazwa jana.

Katika uchaguzi huo utakaofanyika jijini Tanga Agosti 7, mwaka huu, jumla ya wagombea wa nafasi ya urais waliochukua fomu walikuwa 10, lakini waliorudisha fomu walikuwa sita, huku waliopita katika mchujo huo wa awali wakiwa ni watatu ambao ni Hawa Mniga, Evans Mgeusa na Wallace Karia, anayetetea nafasi hiyo wakati Ally Mayay, Ally Saleh 'Alberto' na Oscar Oscar wakienguliwa.

Hata hivyo, baada ya kutangazwa kuenguliwa, Alberto, alisema hajaridhika na uamuzi huo, hivyo anasubiri kwanza majibu ya barua waliyopeleka kwa msajili wa vyama, kusimamisha mchakato hadi kanuni zipitiwe upya.

"Hatuwezi kusema lolote kwa sasa, kesho (leo) tutaenda kwa msajili wa vyama kufuatilia majibu ya barua, baada ya majibu hayo ndio nitaweka msimamo," alisema Alberto.

Kwa upande wa Mayay, alisema: "Kesho (leo), nitaweka wazi msimamo wangu kuhusu kuondolewa jina langu katika mchujo wa kuendelea na mchakato wa uchaguzi."

Awali, akizungumza na waandishi wa habari katika Makao Makuu ya TFF jijini Dar es Salaam jana wakati wa kutangaza matokeo hayo, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya uchaguzi, Benjamin Kalume, alisema walipitia fomu zote na kufanya mchujo kwa kuzingatia kanuni za uchaguzi wa shirikisho hilo.

Alisema wagombea hao watatu wamefanikiwa kupita katika mchujo huo baada ya kukamilisha vigezo ikiwamo kupata wadhamini ambapo Karia alipata 'Endorsement' (wadhamini) 18, Hawa ambaye ni mwanamke pekee akipata wadhamini sita huku Mgeusa naye akikidhi idadi ya wadhamini ambapo kanuni inasema angalau kupata watano.

"Watatu kati ya sita waliorudisha fomu, hawakupita katika mchujo huo ni Mayay alikuwa na mdhamini mmoja tofauti na kanuni ikihitaji watano na kushindwa kukamilisha baadhi ya fomu ikiwa haikuthibitishwa vyeti kwa Kamishna wa Viapo.

"Oscar Oscar hakupata mdhamini, Ally Saleh hakuwa na mdhamini, lakini vyeti vyake naye havikupita kwa Kamishna wa Viapo, kwa sababu hizo wahawakuwa na sifa za kuendelea katika mchakato huo," alisema Kalume.

Alisema kwa upande wa wagombea nafasi ya wajumbe waliopita katika mchujo huo wanaowania nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Utendaji ya TFF, kwa kanda zote sita; Kanda namba moja (Dar es Salaam, Lindi, Morogoro, Mtwara na Pwani), waliochukua fomu ni saba na watatu wamefanikiwa kupita katika mchujo kwa kukidhi vigezo ambao ni Athuman Kambi, Lameck Nyambaya na Hosseah Lugano.

Walioenguliwa kwa maelezo ya kutokidhi vigezo ni Ellisony Mweladzi, Jimmy Shomari, Liston Katabazi na Saady Khimji ambaye alipata mdhamini kupitia klabu ya Yanga wakati anatakiwa mdhamini wake kutoka ngazi ya mkoa.

Kalume alisema Kanda namba mbili (Mkoa wa Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga) walikuwa watatu na waliopita ni Khalifa Abdallah na Zakayo Mjema huku Thabiti Kandoro akiondolewa kwa sababu hajakidhi vigezo ikiwamo kupata mdhamini wa klabu na si mkoa.

"Kanda namba tatu (Mkoa wa Iring, Mbeya, Njombe, Ruvuma na Songwe, waliopita ni Aboufian Sillia, James Mhagama na Mohammed Mashango, ambao hawakupita ni Ulisaja Elias, Denis Manungu na Joseph Ngunangwa ambao hawakukidhi vigezo.

"Waliopita kwa Kanda namba nne (Mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Simiyu na Singida) ni Hamis Kitila, Mohammed Aden na Osuri Kosuri huku Mrisho Ramadhani akiondolewa katika mchujo huo kutokana na kutokidhi vigezo," alisema.

Aidha, Kalume alitaja wagombea watatu wote wamepita kwa upande wa Kanda namba tano (Mikoa ya Geita, Kagera, Mara na Mwanza ambao ni Salum Chama, Vedastus Lufano na Salum Alli huku kwa Kanda namba sita nao pia kipita wote watatu ambao ni Blassy Kiondo, Issa Mrisho na Kenneth Pesambili.

"Baada ya mchakato huu sasa tunaenda kwenye hatua ya kuweka na kuwekewa pingamizi kwa waliopita katika mchakato huo na zoezi hilo linaanza Juni 19 hadi 21, baada ya hapo Juni 22 hadi 24 kusikiliza pingamiza hizo na Juni 25 hadi 27 tutakuwa na zoezi la usahili," alisema makamu mwenyekiti huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002